Haliuzwi
MACHI 21, 2026
/islamicftz
Shawwal 2 1447
IMAAN
ISSN 5618 - NO. 576
Huwatoa watu gizani kwa idhini ya Allah

Al-Aqsa yafungwa siku ya Eid, Waislamu Jerusalem waswali nje

Wito Eid el Fitri: Mema ya Ramadhan yaendelezwe

Dkt. Mwinyi: Roho ya kusaidiana iendelee hata baada ya mfungo

Sheikh Lipena: Mawasiliano ya hekima iwe nyenzo yetu kukuza uelewano wa kitaifa

Aref Nahdi: Msilegeze misingi ya dini baada ya Ramadhan

Wapalestina Gaza waadhimisha Eid al-Fitr licha ya majeraha ya vita

1,109 idadi ya misikiti kati ya 1,244 iliyoharibiwa miaka miwili iliyopita

72,000 Idadi ya Wapalestina waliouawa na mashambulizi ya Israel miaka miwili iliyopita

171,000 Idadi ya Wapalestina waliojeruhiwa na mashambulizi ya Israel huko Gaza miaka miwili iliyopita

Rais Samia ahimiza amani, umoja na kuvumiliana kidini

Wapalestina katika swala ya Eid al-Fitr Ijumaa tarehe 20 Machi 2026 katika eneo la Tel al-Hawa, Gaza.

Nchi 12 za Kiarabu na Kiislamu zaitaka Iran kusitisha mashambulizi

شوّال

MATUKIO KATIKA PICHA

Na abdulrahman Omar
0655 763 580

Morogoro: Maadhimisho ya sikukuu ya Eid al-Fitr yaliyofanyika Ijumaa tarehe 20 Machi 2026

شوّال

MATUKIO KATIKA PICHA

Na abdulrahman Omar

0655 763 580

شوّال

HABARI MOROGORO

NA YUSUFU AMINI

Jamii yatakiwa kudumisha amani, mshikamano baada ya Ramadhan

Jamii imetakiwa kuendelea kudumisha amani, upendo na mshikamano hata baada ya kumalizika kwa mwezi mtukufu wa Ramadhan, ili kuhakikisha kuwa matunda ya ibada yanaendelea kuonekana katika maisha ya kila siku.

Wito huo umetolewa leo mkoani Morogoro wakati wa maadhimisho ya sikukuu ya Eid al-Fitr yaliyofanyika katika maeneo mbalimbali ya ibada.

Akitoa khutba ya Eid, Sheikh Mikidad Lipena alisema kuwa amani ndiyo msingi mkuu unaowezesha jamii kuishi kwa utulivu na kufanya ibada kwa uhuru. Alisisitiza umuhimu wa kuendeleza maadili, ikiwemo haki, uadilifu na upendo, ambayo waumini wamejifunza katika kipindi chote cha Ramadhan.

Aidha, Sheikh Mikidad Lipena aliwataka viongozi wa dini kuwa kiunganishi kizuri kati ya wananchi na viongozi wa serikali kwa kutumia lugha ya hekima na staha. Alieleza kuwa jukumu la kujenga jamii bora linawahusu pia wanawake, ambao wana nafasi kubwa katika malezi na ustawi wa familia na jamii kwa ujumla.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Taasisi ya The Islamic Foundation, Aref Nahdi, aliunga mkono maelekezo hayo kwa kuwahimiza waumini kuendelea kushikamana na kuenzi misingi ya dini hata baada ya kumalizika kwa mfungo.

Sanjari na hilo, Mwenyekiti huyo alitumia fursa hiyo kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa uongozi bora na madhubuti katika kuwaletea maendeleo wananchi.

Kwingineko katika viwanja vya Ma'ahad Imaan Msamvu, Khatibu wa swala ya Eid, Sheikh Abdulrahmani Muhammad, aliwataka Waislamu kuwaombea viongozi wa nchi ili kudumisha amani, utulivu na maendeleo ya taifa.

Waislamu mkoani humo walijitokeza kwa wingi kushiriki swala ya Eid tangu alfajiri, wakionesha mshikamano mkubwa kwa kukusanyika pamoja katika ibada.

Kwa ujumla, maadhimisho ya Eid mkoani Morogoro yamebeba ujumbe wa kuimarisha umoja, mshikamano na kudumisha amani katika jamii.

شَوَّال

MATUKIO KATIKA PICHA

Na abdulrahman Omar
0655 763 580

Morogoro: Maadhimisho ya sikukuu ya Eid al-Fitr yaliyofanyika Ijumaa tarehe 20 Machi 2026

شوّال

HABARI

DAR ES SALAAM

NA MWANDISHI WETU

Rais Samia ahimiza amani, umoja na kuvumiliana kidini

Kwenye salamu zake kwenye Baraza la Idd el Fitr lilifanyika katika Ukumbi wa Mwalimu Nyerere jana jioni, Rais Samia alisema Serikali itaendelea kulinda uhuru wa kila Mtanzania kuabudu kulingana na imani yake, huku akisisitiza umuhimu wa kuheshimu mipaka ya uhuru huo ili kudumisha amani na mshikamano wa taifa.

Alisema Serikali inatambua na kuheshimu haki ya msingi ya uhuru wa kuabudu, lakini akaonya kuwa uhuru huo unapaswa kutumika kwa kuwajibika.

"Nataka niwahakikishie kuwa Serikali yetu itaendelea kutimiza wajibu wake wa kikatiba wa kulinda uhuru wa kila Mtanzania kuabudu kulingana na imani yake. Pamoja na hayo, ni muhimu kwetu sote kuheshimu mipaka ya uhuru huo," alisema.

Aliongeza kuwa: "Hatuna budi kuheshimu sheria za nchi na haki za wengine ili uhuru huo (wa kuabudu) usigeuke kuwa chanzo cha chuki, mgawanyiko au kuvuruga amani na mshikamano wa taifa letu."

Alisema ni wajibu wa kila mwananchi kuhakikisha kuwa matumizi ya uhuru huo hayakiuki sheria za nchi wala haki za wengine.

Aidha, Rais Samia alitoa wito kwa Watanzania kuendelea kuenzi umoja, mshikamano na kuvumiliana kidini, akibainisha kuwa misingi hiyo ndiyo nguzo muhimu ya kudumisha amani na utulivu wa nchi.

Alikemea matumizi mabaya ya akili mnemba, akisema inapotumika vibaya kwa kuwatukana viongozi wa Serikali na wa dini inaweza kuhatarisha mustakabali wa taifa.

"Watoto wakiona mambo hayo, nchi haitakuwa salama. Haitatulia, na maendeleo hayatakuwepo kwa sababu kutakuwa na vurugu. Viongozi wa dini endeleeni na jukumu hili muhimu la kuwajenga wananchi na kuwaelekeza ili tuwe na taifa lenye amani, utulivu na ustahimilivu, na hivyo kujenga kizazi bora cha sasa na kijacho," alisema.

Alisema katika nyakati hizi ambazo dunia inashuhudia migogoro katika maeneo mbalimbali, Tanzania imeendelea kubaki salama na yenye amani, jambo linalopaswa kuthaminiwa kwani si kila mtu anatamani kuona hali hiyo ikiendelea. Hivyo, alisisitiza umuhimu wa kuimarisha mshikamano na kuendeleza upendo kwa nchi na taifa.

Pia, alitumia nafasi hiyo kulitaka Baraza la Kiislamu Tanzania (Bakwata) kujiandaa vizuri kuhakikisha uchaguzi wao unaotarajiwa kufanyika mwaka huu unakuwa wa haki na amani.

Mapema, Rais wa Zanzibar, Dk Hussein Mwinyi, aliwataka wananchi kudumisha mshikamano, umoja na mema waliyoyatekeleza wakati wa mfungo wa mwezi Mtukufu wa Ramadhani, kwa kuzingatia maslahi ya taifa na ustawi wa jamii.

"Tumetekeleza ibada ya swaumu katika hali ya amani na utulivu. Hii ni neema kubwa, kwani wapo Waislamu wengi, hususan Mashariki ya Kati, wanaokabiliana na changamoto za kiusalama," alisema Rais Mwinyi baada ya swala ya Idd mjini Unguja.

"Ni wajibu wetu kuendeleza mema haya katika maisha yetu ya kila siku ili kupata mafanikio duniani na kesho mbele ya haki. Tumwombe Mwenyezi Mungu atuwezeshe kudumu katika mwenendo huu mwema," alisema.

Rais Mwinyi pia ameyataja baadhi ya mema yaliyotekelezwa na wananchi, ikiwamo kufanyiana hisani na kutoa sadaka kwa wenye uwezo mdogo ili kuwasaidia kukidhi mahitaji yao.

"Sadaka hizo zimesaidia kuhakikisha mahitaji ya wengi yanatimizwa, kuondoa wasiwasi wa kupata futari na kusaidia watu kutekeleza ibada ya swaumu, huku zikichangia kuimarisha mapenzi na mshikamano kati yetu," alisema.

Ilikusherehekeasikukuukwaamaninafuraha, Rais Mwinyi amezitaka mamlaka zinazohusika na usalama wa viwanja vya sherehe kuhakikisha usalama unadumishwa.

شَوَّال

HABARI ZANZIBAR

NA MWANDISHI WETU

Mwinyi: Roho ya kusaidiana iendelee hata baada ya mfungo

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Alhaj Dkt. Hussein Ali Mwinyi, amewanasihi waumini wa dini ya Kiislamu na jamii kwa ujumla kuendeleza utaratibu mzuri wa kuwasaidia na kuwahurumia watu wasio na uwezo kwa kuzingatia mahitaji yao maalumu.

Alhaj Dkt. Mwinyi ameyasema hayo katika Baraza la Eid el-Fitri lililofanyika katika Ukumbi wa Chuo cha Polisi, Ziwani, Mkoa wa Mjini Magharibi.

Amefafanua kuwa ili kuwa na jamii yenye ustawi bora, ni vema utaratibu huo ukaendelezwa kwani kwa kiasi kikubwa umewasaidia watu wa makundi maalumu, wakiwemo mayatima, wajane na mafakiri, kupata futari na kutekeleza ibada ya funga kikamilifu.

Aidha, Alhaj Dkt. Mwinyi amesema waumini wa dini ya Kiislamu wana wajibu mkubwa wa kutekeleza na kuendeleza mambo yote ya kheri yaliyokuwa yakifanyika katika Mwezi Mtukufu wa Ramadhani, ikiwemo kumcha Mwenyezi Mungu kwa bidii, kwani yanaongeza upendo, umoja na mshikamano.

Akizungumzia Sikukuu ya Eid el-Fitri, amelitaka Jeshi la Polisi kusimamia na kuhakikisha usalama na amani vinaimarishwa katika viwanja vya sikukuu, pamoja na kusisitiza usimamizi madhubuti wa sheria za usalama barabarani ili kuhakikisha wananchi wanasherehekea sikukuu kwa amani na utulivu.

Kwa upande wa suala la Hijjah, amesema Serikali itaendelea kushirikiana na taasisi zinazosafirisha mahujaji kupitia Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana ili kuhakikisha Waislamu wanaokwenda kutekeleza ibada ya Hijjah wanaongezeka. Aidha, ameeleza kuwa Serikali inaendelea na utaratibu wa kukamilisha kuanzishwa kwa mfuko maalum wa Hijjah.

Baraza la Eid limehudhuriwa na Mke wa Rais wa Zanzibar, Mhe. Mama Mariam Mwinyi, viongozi mbalimbali wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, akiwemo Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Mhe. Hemed Suleiman Abdulla, Rais Mstaafu wa Zanzibar, Dkt. Ali Mohammed Shein, Makamu wa Pili wa Rais Mstaafu, Balozi Seif Ali Iddi, Mufti Mkuu wa Zanzibar, Sheikh Saleh Omar Kaabi, Spika wa Baraza la Wawakilishi, Mhe. Zuberi Ali Maulid, pamoja na viongozi wa dini, masheikh na waumini mbalimbali.

MAKALA MAALUM

SHEIKH
Shaaban Mussa
0786 272 323

Nini suluhu ya changamoto za mwandamo, mjadala unaojirudia kila mwaka

Mwandamo wa mwezi ni suala lenye umuhimu mkubwa kwa Waislamu ambao tunategemea kalenda ya Hijriya katika kuanza na kumaliza ibada kama Ramadhan, Idd nk.

Hata hivyo, kila mwaka hujitokeza mjadala na hali ya kutofautiana kuhusu uthibitisho wa kuandama kwa mwezi mpya. Mjadala huu mara nyingi huambatana na taarifa zinazokinzana, tafsiri tofauti za kimaandiko na kisayansi, na wakati mwingine hisia kali za kijamii.

Asili ya tofauti za mwandamo Tofauti za kijiografia

Mwezi hauonekani katika majira mamoja duniani kote. Nchi moja inaweza kuuona mwezi mpya ilhali nyingine bado haijaweza kuuona kutokana na tofauti za muda wa machweo na mawio, hali ya anga kama mawingu, vumbi au unyevunyevu na pia latitudo na nafasi ya kijiografia ya eneo husika.

Mbinu za uthibitisho wa mwezi

Kwa ujumla, kuna njia kuu zinazotumika katika kuthibitisha kuandama kwa mwezi zikiwemo kwanza, kuuona mwezi kwa macho au kwa msaada wa vifaa; ushahidi wa mashahidi au taarifa kutoka kwa watu waliouona mwezi au kukamilisha siku 30 – endapo mwezi haujaonekana au hakuna ushahidi ulio thibitishwa kwa wakati. Tofauti katika matumizi ya mbinu hizi husababisha hitilafu za kiutendaji kila mwaka.

Tofauti za mamlaka za uthibitisho

Uamuzi wa kuanza au kumaliza mwezi hutolewa na mamlaka tofauti kulingana na nchi au jamii, zikiwemo serikali, kamati au mabaraza ya kidini au wanazuoni na taasisi za Kiislamu. Kutokana na hali hii, uamuzi unaweza kutofautiana hata ndani ya jamii moja, hasa pale ambapo mifumo ya utoaji wa taarifa na uthibitisho siyo ya aina moja na hivyo haifanani.

Athari za taarifa zinazokinzana

Kila inapofika mwisho wa mwezi wa 29 au 30 wa kalenda ya Hijriya, mara nyingi hujitokeza taarifa tofauti kama mwezi haujaonekana katika maeneo fulani, mwezi umeonekana katika nchi au maeneo mengine, kilichoonekana haukuwa mwezi na taarifa zisizo rasmi kuenea kwa kasi mitandaoni,

Hali hii huweza kusababisha kuchanganyikiwa kwa umma, kugawanyika kwa kuanza au kumaliza ibada na tofauti za kimtazamo ndani ya jamii.

Nafasi ya mitandao ya kijamii

Mitandao ya kijamii kwa sasa imekuwa chanzo kikubwa cha taarifa, lakini pia chanzo cha upotoshaji. Changamoto zinazoonekana ni pamoja na usambazaji wa haraka wa taarifa zisizo rasmi upotoshaji wa picha au ushahidi na watu wasio na mamlaka kutoa matamko ya mwisho.

Hali hii ya mkanganyiko wa taarifa katika mitandao huongeza sintofahamu, hasa katika kipindi cha mabadiliko ya mwezi.

Uhusiano kati ya dini, sayansi na uongozi

Mjadala wa mwandamo wa mwezi hujumuisha maeneo matatu muhimu kwanza, dini (Wanazuoni hutegemea maandiko na tafsiri za kisheria kuhusu uthibitisho wa mwezi), sayansi (baadhi ya wataalamu wa falaki wanao uwezo wa kutoa utabiri sahihi kuhusu uwezekano wa kuonekana kwa mwezi mpya kulingana na hesabu za anga).

Eneo la tatu ni uongozi wa jamii, yaani serikali na taasisi za kidini hujaribu kuleta uamuzi wa pamoja ili kuhakikisha umoja na kupunguza migawanyiko ya kijamii. Changamoto hutokea pale ambapo tafsiri au matokeo ya vipengele hivi hayalingani.

Changamoto ya uaminifu na taarifa bandia

Katika baadhi ya matukio, hujitokeza madai yasiyo na uthibitisho wa kutosha kuhusu kuonekana kwa mwezi katika maeneo mbalimbali.

Hali hii husababisha watu kuamini taarifa zisizo sahihi, kujitokeza migogoro kuhusu nani ameona au hajaona mwezi na shinikizo kwa mamlaka kufanya maamuzi ya haraka bila uhakiki wa kina. Ni muhimu kusisitiza kuwa uthibitisho wa mwezi unahitaji ushahidi uliohakikiwa na mamlaka husika, si taarifa za mdomo au mitandao pekee.

Mapendekezo ya suluhisho

Ili kupunguza changamoto zinazojitokeza kila mwaka, hatua kadhaa zinaweza kusaidia, ikiwemo kwanza, kuimarisha taasisi za uthibitisho wa mwezi na kuanzisha na kuimarisha kamati zenye mchanganyiko wa wanazuoni na wataalamu wa falaki ili kufanya maamuzi yenye mshikamano zaidi.

شوّال

HABARI MASHARIKI YA KATI

NA MWANDISHI WETU

Wapalestina Gaza waadhimisha Eid al-Fitr licha ya majeraha ya vita

Zaidi ya Wapalestina 72,000 wauawa huku Gaza ikiadhimisha Eid katikati ya majeraha ya vita

Baada ya zaidi ya miaka miwili ya mashambulizi ya Israel katika Ukanda wa Gaza, zaidi ya Wapalestina 72,000 wameuawa na zaidi ya 171,000 kujeruhiwa, kwa mujibu wa Wizara ya Afya ya Gaza. Katikati ya hasara hizi kubwa, wakazi wanaadhimisha Eid al-Fitr, sikukuu ya kumaliza mfungo wa mwezi mtukufu wa Ramadhani.

Sherehe nne zilizopita za Eid mjini Gaza zimekuwa zikigubikwa na sauti za ndege za kivita, milio ya risasi na mashambulizi ya makombora. Ingawa Eid ya mwaka huu imewadia bila sauti hizo za vita ambazo wakazi walizoea, dalili za furaha bado ni chache. Maelfu ya familia zimepoteza makazi na wapendwa wao, huku wengi wakiishi katika makazi ya muda au kwenye vifusi vya nyumba zao, hali iliyobadili desturi na mwenendo wa kawaida wa sikukuu hiyo.

Kabla ya vita, asubuhi za Eid Gaza zilijaa waumini waliokuwa wakimiminika misikitini kwa ajili ya swala ya Eid. Hata hivyo, taratibu hizi zimebadilika kwa kiasi kikubwa kufuatia mashambulizi ya Israel yaliyoathiri pia maeneo ya ibada. Kwa mujibu wa Wizara ya Wakfu na Masuala ya Kidini Gaza, misikiti 1,109 kati ya 1,244 imeharibiwa kabisa au kwa sehemu tangu kuanza kwa vita Oktoba 2023, na kufanya mingi kutoweza kutumika.

Kutokana na hali hiyo, wakazi wamelazimika kuswali katika maeneo madogo ya wazi, barabarani au ndani ya mahema katika kambi za wakimbizi, hali inayoonyesha jinsi vita ilivyobadili hata ibada za kidini zilizozoeleka kwa muda mrefu.

Imamu wa Msikiti wa Mashahidi wa Al-Aqsa, Mohammad Al-Hajj, amesema maandalizi ya Eid zamani yalianza siku kadhaa kabla, huku waumini wakijitolea kusafisha na kuandaa msikiti kwa ajili ya swala iliyokuwa ikiwakusanya mamia ya wakazi wa eneo hilo. Ameongeza kuwa watoto walifika alfajiri wakiwa wamevaa mavazi mapya, wakisubiri swala kuanza katika mazingira ya furaha na utulivu.

Hata hivyo, amesema taswira hiyo imebadilika kwa kiasi kikubwa kutokana na uharibifu na wakazi kuhama makazi yao. Licha ya hayo, wakazi bado wanajitahidi kuendeleza ibada zao. "Licha ya yote yaliyotokea, watu wameazimia kuswali na kusherehekea Eid, hata kama sasa inafanyika katika maeneo madogo au kati ya mahema," amesema.

Wapalestina katika swala ya Eid al-Fitr Ijumaa tarehe 20 Machi 2026 katika eneo la Tel al-Hawa, Gaza.

شوّال

HABARI MASHARIKI YA KATI

NA MWANDISHI WETU

Al-Aqsa yafungwa siku ya Eid, Waislamu Jerusalem waswali nje

Ripoti hiyo inaeleza kuwa mamia ya waumini walikusanyika karibu na kuta za Mji Mkongwe wa Jerusalem na kuswali katika barabara na maeneo ya karibu baada ya kuzuiwa kuingia ndani ya msikiti huo, ambao ni moja ya maeneo matakatifu zaidi katika Uislamu

Mamia ya Waislamu mjini Jerusalem wamelazimika kuswali swala ya Eid nje ya lango la Msikiti wa Al-Aqsa baada ya mamlaka za Israel kuufunga msikiti huo kwa waumini, tukio lililozua huzuni na hasira miongoni mwa Wapalestina.

Kwa mujibu wa ripoti ya The Guardian, hii ni mara ya kwanza tangu mwaka 1967 kwa Msikiti wa Al-Aqsa kufungwa kwa waumini wa Kiislamu wakati wa sikukuu ya Eid al-Fitr, hatua iliyotokana na kile mamlaka za Israel zilisema ni sababu za kiusalama zinazohusiana na mvutano wa kijeshi katika eneo hilo.

Ripoti hiyo inaeleza kuwa mamia ya waumini walikusanyika karibu na kuta za Mji Mkongwe wa Jerusalem na kuswali katika barabara na maeneo ya karibu baada ya kuzuiwa kuingia ndani ya msikiti huo, ambao ni moja ya maeneo matakatifu zaidi katika Uislamu.

Mkaazi mmoja wa Jerusalem, Hazen Bulbul, alinukuliwa na The Guardian akisema siku hiyo ilikuwa "siku ya huzuni kubwa kwa Waislamu wa Jerusalem," akihofia kuwa hatua hiyo inaweza kuwa mwanzo wa vizuizi zaidi katika siku zijazo.

Kwa mujibu wa The Guardian, hatua hiyo pia imekosolewa na mashirika kadhaa ya kimataifa ikiwemo Umoja wa Nchi za Kiarabu na Jumuiya ya Ushirikiano wa Kiislamu (OIC), ambayo yamesema kufungwa kwa msikiti huo kunakiuka uhuru wa ibada na haki za kidini.

Mvutano kuhusu eneo la Al-Aqsa umeongezeka katika miezi ya karibuni, huku Wapalestina wakisema vizuizi vya kuingia katika eneo hilo vinaendelea kuongezeka na kuzidisha hali ya taharuki katika mji wa Jerusalem.

شَوَّال

HABARI
MASHARIKI YA KATI

NA MUGINI SINGIRA

Nchi 12 za Kiarabu na Kiislamu zaitaka Iran kusitisha mashambulizi

Nchi 12 za Kiarabu na Kiislamu zimetoa wito kwa Iran kusitisha mara moja mashambulizi na vitendo vya uchokozi vinavyoweza kuvuruga usafirishaji wa mafuta na biashara katika Mlango wa Hormuz (Strait of Hormuz), njia muhimu ya kimataifa ya usafiri wa nishati.

Kwa mujibu wa taarifa iliyoripotiwa na Moneycontrol, mataifa hayo yalisisitiza katika tamko la pamoja kuwa mashambulizi yanayohusishwa na Iran yanaweza kuhatarisha usalama wa eneo la Mashariki ya Kati pamoja na uchumi wa dunia unaotegemea sana usafirishaji wa mafuta kupitia njia hiyo.

Katika tamko hilo, nchi hizo zilitoa wito wa "kusitishwa mara moja kwa mashambulizi yote" na kuepukwa kwa vitisho au hatua zozote zinazoweza kuathiri usalama wa meli na biashara katika mlango huo wa bahari.

Mlango wa Hormuz ni mojawapo ya njia muhimu zaidi za usafirishaji wa mafuta duniani, ambapo sehemu kubwa ya mafuta na gesi inayouzwa kimataifa hupitia katika eneo hilo. Wataalamu wa nishati wanaonya kuwa kuvurugika kwa njia hiyo kunaweza kusababisha kupanda kwa bei ya mafuta na kuathiri uchumi wa mataifa mengi.

Nchi hizo pia zilisisitiza umuhimu wa kuheshimu sheria za kimataifa, uhuru wa usafiri wa majini na utatuzi wa migogoro kwa njia ya diplomasia. Kwa mujibu wa taarifa hiyo, viongozi hao walionya kuwa kuendelea kwa mvutano katika eneo hilo kunaweza kuathiri usalama wa kikanda na kuharibu juhudi za kuleta utulivu wa kisiasa na kiuchumi katika Mashariki ya Kati.

HABARI
MASHARIKI YA KATI

NA MWANDISHI WETU

Saudi Arabia yaweka mwongozo kurahisisha kurejea mahujaji wa Umrah

Serikali ya Saudi Arabia imetangaza hatua mpya za kurahisisha taratibu za kuondoka kwa mahujaji waliotekeleza ibada ya Umrah huku msimu huo ukikaribia kumalizika.

Kwa mujibu wa taarifa iliyoripotiwa na Arab News, Wizara ya Hajj na Umrah imetoa mwongozo maalumu unaolenga kuhakikisha usafiri wa mahujaji unaondoka kwa utaratibu katika viwanja vya ndege na vituo vingine vya usafiri nchini humo.

Ripoti hiyo inaeleza kuwa hatua hizo zimechukuliwa ili kupunguza msongamano katika bandari na viwanja vya ndege wakati mahujaji wanaporejea katika nchi zao baada ya kukamilisha ibada. Kwa mujibu wa Arab News, wizara hiyo imewasisitiza mahujaji kufuatilia taarifa rasmi kutoka viwanja vya ndege na mashirika ya ndege pamoja na kuthibitisha ratiba za safari kabla ya kuelekea uwanjani ili kuepuka usumbufu wa safari.

Wizara hiyo pia imeelekeza mahujaji kuratibu safari zao na kampuni za Umrah na mashirika ya ndege ili kuhakikisha ratiba za kuondoka zimeidhinishwa na kufuatwa ipasavyo.

Aidha, ripoti hiyo imeongeza kuwa maandalizi ya mapema kama kufunga mizigo kabla ya safari na kufuata masharti ya mizigo ya mashirika ya ndege yanaweza kusaidia kupunguza ucheleweshaji wa taratibu za usafiri.

Kwa mujibu wa wizara hiyo, mahujaji wanaorudi pia wanaruhusiwa kusafirisha maji ya Zamzam ikiwa yatakuwa yamenunuliwa katika vituo rasmi vya viwanja vya ndege na kufungwa kwa kufuata masharti yaliyowekwa, ambapo kila chupa hairuhusiwi kuzidi lita tano.

Hatua hizi zinalenga kuhakikisha mahujaji wanakamilisha safari zao kwa utulivu na ufanisi kadri msimu wa Umrah unavyofikia mwisho wake.

شوّال

HABARI MCHANGANYIKO

NA MWAJUMA SALUM

Viongozi wa Kiislamu Uganda waonya: Bila amani hakuna maendeleo ya uchumi

Viongozi wa Kiislamu nchini Uganda wametoa wito kwa jumuiya ya kimataifa kulinda amani ya dunia wakisisitiza kuwa utulivu wa kisiasa na kijamii ni msingi muhimu wa maendeleo ya kiuchumi. Wito huo ulitolewa na Mufti Mkuu wa Uganda, Sheikh Shaban Ramadhan Mubaje, wakati akizungumzia mvutano unaoongezeka katika maeneo mbalimbali duniani.

Akizungumza katika mkusanyiko wa waumini, Sheikh Mubaje alisema migogoro na vita huathiri kwa kiasi kikubwa ustawi wa uchumi wa mataifa kwa sababu huvuruga biashara, uwekezaji na shughuli za uzalishaji. Alieleza kuwa bila amani, nchi hushindwa kuvutia wawekezaji na kuendeleza miradi ya maendeleo inayohitaji utulivu wa muda mrefu.

Kiongozi huyo wa dini alionya kuwa vita husababisha uharibifu wa miundombinu, kupungua kwa ajira na kuongezeka kwa umasikini, hali inayodhoofisha uwezo wa jamii kujijenga kiuchumi. Kutokana na hali hiyo, aliwataka viongozi wa dunia kutumia diplomasia na mazungumzo kama njia kuu ya kutatua migogoro badala ya kutumia nguvu.

Aidha, alisema taasisi za dini zina nafasi muhimu katika kuhimiza maadili ya amani, mshikamano na uwajibikaji katika jamii. Kwa mujibu wake, mazingira ya amani huwezesha wananchi kufanya kazi kwa tija, kuimarisha biashara na kuongeza ustawi wa kiuchumi wa taifa.

Kauli hiyo ya viongozi wa Kiislamu Uganda inakuja wakati dunia inakabiliwa na migogoro kadhaa ya kisiasa na kijeshi inayotishia utulivu wa uchumi wa kimataifa pamoja na maendeleo ya jamii.

Waislamu wasema wingi wa dini unawafanya wajisikie sehemu ya Uingereza

Baadhi ya Waislamu nchini Uingereza wanasema kuwa uwepo wa dini mbalimbali katika jamii ya Uingereza unawafanya wajisikie zaidi kuwa sehemu ya taifa hilo badala ya kuwafanya wajihisi wageni.

Kwa mujibu wa ripoti ya The Guardian, maoni hayo yalitolewa wakati wa sherehe za Eid al-Fitr zilizofanyika katika Msikiti wa Baitul Futuh kusini mwa London, ambapo maelfu ya Waislamu walikusanyika kusherehekea kumalizika kwa mwezi wa Ramadhani.

Baadhi ya washiriki wa sherehe hizo walisema kuwa utofauti wa kidini ni sehemu muhimu ya utambulisho wa Uingereza ya kisasa. Mmoja wa washiriki, Taufique Ahmad, alinukuliwa na The Guardian akisema kuwa kuona dini mbalimbali zikiheshimiwa katika jamii kunamfanya ajisikie "zaidi kuwa Mwingereza."

Ripoti hiyo inaeleza kuwa mjadala kuhusu nafasi ya Uislamu katika jamii ya Uingereza umeongezeka hivi karibuni baada ya baadhi ya wanasiasa kukosoa ibada za hadhara za Waislamu, wakidai kuwa zinaweza kuonekana kuwa za kutishia au "si za Kiingereza." Kauli hizo zimekosolewa na viongozi wa jamii na wataalamu wa sheria wanaosema zinahatarisha mshikamano wa kijamii.

Kwa mujibu wa The Guardian, viongozi wa jamii wamesisitiza kuwa sherehe na ibada za dini mbalimbali ni sehemu ya maisha ya kila siku nchini humo na zinapaswa kuonekana kama ishara ya jamii yenye uvumilivu na uhuru wa kuabudu.

Familia za Kiislamu zakimbia ghasia za uchaguzi India

Familia kadhaa za Kiislamu zimekimbia makazi yao katika jimbo la Meghalaya kaskazini mashariki mwa India kufuatia ghasia zilizohusishwa na mchakato wa uchaguzi wa serikali za mitaa, tukio lililosababisha vifo na uharibifu wa mali.

Kwa mujibu wa taarifa ya tovuti ya habari 5Pillars, ghasia hizo zilitokea katika wilaya ya West Garo Hills ambapo watu wawili Waislamu waliuawa huku maduka kadhaa na nyumba zikichomwa moto katika mashambulizi yaliyolenga jamii ya Waislamu wenye asili ya Kibengali.

Ripoti hiyo inaeleza kuwa hofu ilianza kuenea baada ya uvumi kusambaa kuwa wagombea Waislamu walikuwa wanajiandaa kugombea katika uchaguzi wa Baraza la Wilaya la Garo Hills (GHADC). Baada ya hali ya taharuki kuongezeka, familia nyingi ziliamua kuondoka mapema asubuhi na kuelekea vijiji vya karibu au jimbo jirani la Assam kwa usalama.

Mkazi mmoja wa eneo hilo alinukuliwa na 5Pillars akisema wanawake na watoto wengi waliondoka kabisa katika maeneo yaliyoathiriwa kwa hofu ya usalama wao.

Katika hatua ya kudhibiti hali hiyo, mamlaka za India ziliweka amri ya kutotoka nje, kusitisha huduma za intaneti kwa muda wa saa 48 na kupeleka wanajeshi kufanya doria katika maeneo yaliyoathiriwa.

Kwa mujibu wa 5Pillars, uchaguzi wa GHADC uliokuwa ufanyike Aprili 10, 2026 umeahirishwa hadi hapo hali ya usalama itakapotengemaa.

Wakati huo huo, familia nyingi za Kiislamu zilizokimbia makazi yao bado hazijarejea, huku wakazi wakisema hali ya hofu na taharuki bado inaendelea katika eneo hilo.

UKHTI FATIMA SS

Salum Awadh atoa mwongozo kwa wawekezaji wachanga wa halal

Wataalamu wa masuala ya uwekezaji wameeleza kuwa mtu yeyote anaweza kuanza kuwekeza hata kwa mtaji mdogo ikiwa ataweka malengo sahihi na kufuata kanuni za msingi za uwekezaji.

Akizungumza katika mwongozo wa uwekezaji uliowasilishwa kwa wawekezaji wanaoanza, Mtendaji Mkuu wa Shirkah Asset Management, Salum Awadh, alieleza kuwa uwekezaji ni mchakato wa kuweka fedha leo kwa matarajio ya kupata faida siku zijazo.

Kwa mujibu wa mwongozo huo, fedha za Kiislamu zinatoa mfumo mbadala wa uchumi unaozingatia sheria za Qur'an, Sunnah, Ijma na Qiyas huku ukiepuka shughuli za kifedha zilizo haramu kama riba, kamari na biashara ya pombe.

Awadh anaeleza kuwa mtu anayetaka kuanza uwekezaji anapaswa kwanza kuweka malengo ya kifedha, kama vile kujenga akiba, kukuza mtaji, kujiandaa kwa kustaafu au kugharamia ibada kama Hajj na Umrah.

Mwongozo huo pia unaeleza kuwa uwekezaji unaweza kufanyika katika maeneo mbalimbali ikiwemo hisa za kampuni, sukuk, majengo, bidhaa za kilimo au mifuko ya uwekezaji inayofuata kanuni za Sharia.

Kwa upande wa soko la hisa Tanzania, mwongozo huo unaonyesha kuwa si kampuni zote zinakidhi vi[illegible] uwek[illegible]ji wa halal, kwani takribani asilimia 70 ya hisa katika soko hilo hazizingatii kanuni za Sharia.

Hata hivyo, Awadh anasisitiza kuwa mtu anaweza kuanza kuwekeza mapema hata kwa kiasi kidogo cha fedha na kuendelea kuongeza uwekezaji wake mara kwa mara huku akifuatilia maendeleo ya uwekezaji wake.

Wataalamu wa uwekezaji wanasema kufuata kanuni kama kuweka malengo, kutawanya uwekezaji na kufuatilia hatari kunaweza kusaidia wawekezaji wapya kujenga utajiri kwa njia endelevu na inayokubalika kidini.

Fursa za uwekezaji wa Halal Nigeria zaongezeka 2026

Wawekezaji wanaotaka kufuata kanuni za fedha za Kiislamu wamehimizwa kuangalia fursa mpya za uwekezaji wa halal nchini Nigeria katika robo ya pili ya mwaka 2026, huku sekta hiyo ikitarajiwa kukua kwa kasi.

Kwa mujibu wa taarifa iliyochapishwa na Zawya, serikali ya Nigeria imeanza kujenga mazingira rasmi ya uchumi wa halal kupitia mkakati wa kitaifa unaolenga kuiwezesha nchi kunufaika na soko la kimataifa la halal linalokadiriwa kufikia takribani dola trilioni 7.7.

Ripoti hiyo inaeleza kuwa mojawapo ya fursa kuu za uwekezaji ni kupitia Sukuk, ambazo ni dhamana za Kiislamu zinazotegemea mali halisi badala ya riba. Sukuk zimekuwa maarufu nchini humo, ambapo toleo moja la dhamana hizo lilivutia maombi ya uwekezaji yenye thamani ya zaidi ya naira trilioni 2.2 kutoka kwa wawekezaji.

Mbali na sukuk, wawekezaji pia wanaweza kuwekeza katika mifuko ya uwekezaji inayofuata Sharia (halal mutual funds), hisa za kampuni zinazokidhi vigezo vya Kiislamu, pamoja na miradi ya kilimo na biashara ndogo ndogo.

Kwa mujibu wa uchambuzi huo, uwekezaji wa halal unavutia zaidi kwa sababu unasisitiza uwazi, uwekezaji katika mali halisi na kugawana faida badala ya mfumo wa riba. Hali hiyo inafanya sekta hii kuvutia wawekezaji wanaotafuta uwekezaji wenye maadili na wenye mchango katika maendeleo ya uchumi.

Wachambuzi wa soko wanasema kuongezeka kwa mifumo ya fedha zisizo na riba kunaweza kusaidia Nigeria kuvutia mtaji zaidi na kuimarisha maendeleo ya sekta mbalimbali za uchumi.

HUDUMA ZA KIFEDHA ZA KIISLAMU

UKHTI FATIMA SS

Qatar yakabiliwa na pigo kubwa kifedha ila ina njia za kujinasua

Qatar inakabiliwa na moja ya changamoto kubwa zaidi za kiuchumi katika eneo la Ghuba kufuatia mashambulizi yaliyoathiri sekta yake muhimu ya gesi asilia, lakini wachambuzi wanasema nchi hiyo bado ina rasilimali za kifedha zinazoweza kusaidia kukabiliana na mshtuko huo.

Kwa mujibu wa uchambuzi wa Reuters Breakingviews, mashambulizi dhidi ya miundombinu ya gesi nchini humo yamepunguza takribani asilimia 17 ya uwezo wa Qatar wa kusafirisha gesi asilia iliyoyeyushwa (LNG), hali inayoweza kusababisha upotevu wa mapato ya karibu dola bilioni 20 kwa mwaka.

Uchambuzi huo unaonya kuwa athari za kiuchumi zinaweza kuwa kubwa zaidi, huku uchumi wa Qatar ukitarajiwa kushuka kwa takribani asilimia 13 mwaka 2026 ikiwa uzalishaji wa gesi utaendelea kuathirika kwa muda mrefu.

Hata hivyo, Reuters Breakingviews inaeleza kuwa Qatar bado ina akiba kubwa ya kifedha inayoweza kusaidia kuimarisha uchumi wake. Benki kuu ya nchi hiyo ina akiba ya karibu dola bilioni 55 pamoja na tani za dhahabu, wakati mfuko wake wa uwekezaji wa taifa una mali zinazokadiriwa kufikia dola bilioni 580 katika uwekezaji duniani.

Kwa mujibu wa uchambuzi huo, mali hizo zinaweza kuuzwa au kutumika kusaidia sekta ya benki na kufidia mapato yaliyopotea kutokana na kupungua kwa mauzo ya gesi.

Wataalamu wa uchumi wanasema uwezo wa Qatar kutumia akiba yake kubwa ya kifedha unaweza kusaidia kupunguza athari za mgogoro wa sasa wa nishati katika eneo la Ghuba, ingawa hatari ya kupanuka kwa vita bado inaweka shinikizo kwa uchumi wa nchi hiyo.

Mamilionea wahamiaji wawa chachu ajira usimamizi wa mali Mashariki ya Kati

Soko la huduma za usimamizi wa mali (wealth management) katika eneo la Mashariki ya Kati na Afrika Kaskazini (MENA) linatarajiwa kukua kwa kasi katika miaka ijayo, likichochewa na uhamaji wa watu matajiri na sera rafiki za uwekezaji katika baadhi ya nchi za Ghuba.

Kwa mujibu wa ripoti mpya ya soko la usimamizi wa mali ya MENA ya mwaka 2026–2031 iliyotolewa na GlobeNewswire, sera za makazi zisizotoza kodi ya mapato katika nchi kama Falme za Kiarabu (UAE) zimekuwa kivutio kikubwa kwa watu wenye utajiri mkubwa duniani. Ripoti hiyo inaeleza kuwa UAE peke yake inatarajiwa kupokea takribani mamilionea 9,800 wanaohamia nchini humo mwaka 2025.

Ripoti hiyo inaeleza kuwa ongezeko la watu hawa wenye utajiri mkubwa linaongeza mahitaji ya huduma za kitaalamu za kusimamia mali, ikiwa ni pamoja na ushauri wa uwekezaji, usimamizi wa mali za familia na upangaji wa kifedha wa kimataifa.

Aidha, Kituo cha Fedha cha Kimataifa cha Dubai (DIFC) kimeripoti kupokea zaidi ya maombi 200 ya kuanzishwa kwa ofisi za familia (family offices) mwaka 2024, ongezeko la asilimia 40 ikilinganishwa na mwaka uliotangulia.

Kwa mujibu wa uchambuzi huo, ushindani kati ya vituo vya fedha kama Dubai na Riyadh unatarajiwa kuimarisha zaidi sekta ya huduma za kifedha katika eneo hilo, huku taasisi za fedha zikiongeza uwekezaji katika teknolojia na huduma mpya ili kuvutia wawekezaji wa kimataifa.

Fintech yatajwa kuwa daraja kati ya ESG na fedha za Kiislamu

Teknolojia za kifedha (fintech) zinaelezwa kuwa chombo muhimu kinachoweza kuunganisha kwa karibu zaidi mfumo wa uwekezaji unaozingatia mazingira, jamii na utawala bora (ESG) na fedha za Kiislamu. Wachambuzi wanasema mifumo hii miwili ina misingi inayofanana, lakini kuziunganisha kikamilifu bado ni changamoto.

Uchambuzi uliochapishwa na Finextra unaeleza kuwa kanuni za msingi za fedha za Kiislamu—kama kuepuka riba (riba), kuepuka biashara hatarishi na kuwekeza katika shughuli zenye manufaa kwa jamii—zinafanana kwa kiasi kikubwa na falsafa ya ESG inayosisitiza uwajibikaji wa kijamii na mazingira.

Hata hivyo, Finextra inaeleza kuwa licha ya kufanana kwa kanuni, uelewa wa fedha za Kiislamu bado ni mdogo katika baadhi ya masoko. Utafiti uliotajwa katika makala hiyo unaonyesha kuwa asilimia 59 ya Waislamu nchini Uingereza na asilimia 64 ya watu wasio Waislamu hawajui kuhusu huduma za benki za Kiislamu.

Kwa mujibu wa Finextra, fintech inaweza kusaidia kupanua uelewa na matumizi ya mfumo huo kwa kutoa majukwaa ya kidijitali yanayorahisisha upatikanaji wa bidhaa za kifedha zinazofuata Sharia. Teknolojia hizo pia zinaweza kuongeza uwazi na kusaidia kufuatilia athari za kijamii na kimazingira za uwekezaji.

Na Said Rajab
0783 650 803

Hawa ndiyo washindi wa mwezi wa Ramadhan



Ndugu zangu katika imani, Ramadhan si mwezi wa kawaida; ni soko la kutafuta mafanikio ya Akhera. Sasa nani miongoni mwetu amepata faida, na nani amepata hasara? Katika mwezi wa Ramadhan, daraja za waja hunyanyuliwa na hadhi huinuliwa, madhambi hufutwa, makosa huoshwa, na matendo mabaya huondolewa.

Hawa ndiyo washindi wa mwezi wa Ramadhan

Ndugu zangu katika imani, Ramadhan si mwezi wa kawaida; ni soko la kutafuta mafanikio ya Akhera. Sasa nani miongoni mwetu amepata faida, na nani amepata hasara? Katika mwezi wa Ramadhan, daraja za waja hunyanyuliwa na hadhi huinuliwa, madhambi hufutwa, makosa huoshwa, na matendo mabaya huondolewa.

Ndani ya Ramadhan, matokeo ya milele huandikwa, amri hubadilishwa na dua hujibiwa. Baadhi yetu tumeiaga Ramadhan huku nyoyo zetu zikiwa zimeoshwa kwa machozi na toba ya kweli kwa Mwenyezi Mungu, na wengine tumeiaga tukiwa na nyoyo ngumu kama zilivyokuwa awali, au pengine zimekuwa ngumu zaidi.

Mtume (rehema za Allah na amani zimshukie) amesema: "Pua yake isuguliwe kwenye vumbi yule ambaye Ramadhan inaingia na kuondoka bila yeye kusamehewa." [Sunan Tirmidhi, hadith namba 3545].

Na Waarabu walitumia msemo "pua yake isuguliwe kwenye vumbi" kumuelezea mtu aliyepata fedheha au hasara kubwa. Hili ni onyo zito linalomaanisha kunyimwa. Ni aibu kiasi gani kwa mtu anayepewa Ramadhan, halafu inaondoka bila yeye kusamehewa! Ni fedheha gani kubwa zaidi kuliko Ramadhan kupita, halafu madhambi yetu yabaki?

Ni hasara gani inayoumiza zaidi kuliko kufunga, kusali na kusoma Qur'an ndani ya mwezi Mtukufu wa Ramadhan, lakini bado hatujabadilika hata kidogo kitabia na mwenendo?

Mwenyezi Mungu atulinde kutokana na hasara ya Ramadhan hii, na atufanye tuwe miongoni mwa washindi na waliofanikiwa. Sasa ni nani washindi wa mwezi wa Ramadhan? Washindi ni wale waliofunga kwa nyoyo zao kabla ya miili yao; waliosimama katikati ya usiku, machozi yakiwatiririka, wakinong'ona: "Ewe Mwenyezi Mungu... nisamehe."

Mshindi ni yule anayevunja kiburi chake, ubinafsi wake, jeuri yake, tabia zake mbaya, pamoja na maneno na kauli zake chafu. Mshindi ni yule anayerekebisha uhusiano uliovunjika, anayerudisha kile alichochukua kinyume cha sharia, au anayemuomba msamaha yule aliyemkosea.

Mshindi ni yule anayetubu bila ya kunuia kurejea tena kwenye madhambi. Mshindi si yule aliyehisi njaa kali katika mchana wa Ramadhan, bali ni yule aliyehisi unyenyekevu mkubwa zaidi na kufanya upya agano lake kwa Mwenyezi Mungu.

Mshindi ni yule ambaye alipohisi njaa alifikiria wale wasiokuwa na chakula wala kinywaji. Mshindi si yule aliyekaa macho kwa muda mrefu zaidi usiku, bali ni yule aliyebadilisha zaidi tabia yake baada ya kumalizika mwezi Mtukufu wa Ramadhan.

Ndugu zangu katika imani, ni akina nani walioshindwa katika mwezi wa Ramadhan? Walioshindwa ni wale waliojizuia kula na kunywa lakini hawakujiepusha na madhambi; walisimama katika safu za sala lakini nyoyo zao hazikujali wala kuathiriwa na kile kilichosomwa na Imam kutoka katika Qur'an.

Walioshindwa ni wale walioisoma Qur'an lakini hawakuwahi kuishi nayo. Mwezi wa Ramadhan umekamilika, nao wakaifunga Qur'an na kuirudisha tena kabatini. Machozi yao yamekauka, toba imekoma, sadaka zimekoma, madhambi ya zamani wameyarudia tena, na tabia mbaya zimeongezeka.

Aliyeshindwa katika Ramadhan ni yule ambaye hajaguswa na Qur'an, hajatikiswa na machozi wala kuzinduliwa na Laylatul Qadri.

Tofauti kubwa kati ya aliyeshinda na aliyepoteza ni kwamba, mshindi anaiacha Ramadhan akiwa na moyo mpya ulioponywa; na aliyeshindwa anaondoka ndani ya Ramadhan kama alivyoingia – moyo wake ukiwa umechakaa kwa madhambi, mgumu kama mwamba, hauitikii Qur'an, haukuathiriwa na ukumbusho, na hurudi kwenye tamaa, matamanio, na matendo yake ya zamani.

Ndugu zangu katika imani, tusiwe miongoni mwa wale waliouza Pepo na msamaha wakati wa Ramadhan kwa sababu ya kutojali, kupuuza, na ujinga.

شوّال

فتاوى

SHEIKH
Shaaban Mussa
0786 272 323

Inajuzu kumlipia mzee wangu aliyefariki deni la Ramadhan?

Swali: **Baba yangu alifariki katika siku za mwisho za Ramadhan, na alikuwa na siku ambazo hakufunga kwa sababu ya ugonjwa na uzee wake. Je, inajuzu mimi kufunga siku hizo badala yake?**

Jawabu: Ikiwa alifariki akiwa katika hali ya ugonjwa wake, basi si lazima wewe ufunge kwa niaba yake na wala haipendezi kufanya hivyo kwa sababu alikuwa na udhuru.

Lakini, ikiwa alipona kisha akapuuza (akaacha kufunga kwa uzembe), basi wewe unaweza kufunga kwa niaba yake; kwa kauli ya Mtume (Allah amshushie rehema na amani): "Yeyote aliyekufa na ana deni la kufunga, atafungiwa na walii wake." Kwa ushahidi wa hadith hii, unawajibika kumlipia. Na kama hukufunga, basi unaweza kulisha maskini kwa kila siku moja.

Lakini ikiwa mzee wako alifariki akiwa katika ugonjwa wake na uzee, na hakuwa na uwezo wa kufunga, basi unatakiwa kulisha maskini kwa kila siku moja, kiasi cha nusu swaa (pishi) kwa kila siku. Ama ikiwa alifariki akiwa katika ugonjwa tu, basi hakuna juu yako kufunga wala kulisha (hakuna fidia inayokupasa). Na Allah ndiye Mjuzi zaidi.

Swali: **Tupeni fatwa kuhusu kizee sana (dhaifu sana), ambaye hawezi kufunga, na pia ni maskini hana kitu chochote. Je, ana wajibu gani?**

Jawabu: Hana wajibu wowote ikiwa ni mnyonge asiyeweza kufunga na pia ni maskini asiyeweza kutoa fidia ya chakula. Hana kufunga wala kulisha kwa sababu Allah amesema: "Mcheni Allah kadiri muwezavyo." [Quran, 64: 16] na pia "Mwenyezi Mungu hamkalifishi mtu isipokuwa kwa kadiri ya uwezo wake." [Qur'an, 2: 286]. Na Allah ndiye Mjuzi zaidi.

Hivyo, kizee huyo hana kufunga wala kulisha kwa sababu ameshindwa vyote viwili na hiyo ni iwapo akili yake bado iko sawa.

Ikiwa mzee huyo amefikia hali ya kupoteza akili (amekosa utambuzi kutokana na uzee), basi hana wajibu wowote hata kama ana mali; kwa sababu ameshaondokewa taklifu (uwajibikaji wa kidini) kwa kupoteza akili.

Swali: **Siwezi kufunga kwa sababu ya ugonjwa ambao umedumu nami kwa muda mrefu, na sikufunga siku kadhaa za Ramadhan iliyopita. Nataka kujua kiasi cha kafara kwa kila siku, na je, kutoa fedha kunaruhusiwa kisheria au la?**

Jawabu: Ikiwa ugonjwa huo hauna matumaini ya kupona kwa mujibu wa makadirio ya madaktari wenye ujuzi, basi inakutosha kutoa chakula kwa kila siku kwa kumlisha maskini mmoja, kiasi cha nusu swaa (pishi) ya tende, mchele, ngano au chakula chochote cha watu wa eneo hilo. Hii ni takriban kilo moja na nusu.

Haitoshelezi kutoa fedha; bali wajibu ni kutoa chakula. Hii inaweza kufanyika kabla au baada ya muda wa kufunga. Inatosha kumpa maskini mmoja au zaidi kwa siku hizo.

Lakini kama ugonjwa una matumaini ya kupona, basi wajibu wako ni kulipa (kufidia) siku ulizokosa kwa kuzifunga baadaye, na hakuna ubaya kuchelewesha qadha mpaka upone, kama Allah alivyosema: "Na mwenye kuwa mgonjwa au safarini basi (afunge) idadi ya siku nyingine." [Qur'an, 2: 186].

Hivyo, Allah ameamuru kufunga siku nyingine badala ya zile alizokosa mgonjwa au msafiri, na hakuamuru kulisha.

Kwa hiyo, ikiwa bado unatarajia kupona na madaktari hawajasema ugonjwa hauponi, basi unapaswa kufunga siku ulizokosa baada ya kupona, hata kama itachukua muda mrefu kama mwaka, miaka miwili au mitatu.

Lakini kama madaktari waliobobea wamesema ugonjwa hauponi na utaendelea, basi inatosha kutoa chakula tu, na hakuna qadha juu yako. Na Allah ndiye Mjuzi zaidi.

شوال

Msamvu, Morogoro
P.O.Box 6011
Morogoro, Tanzania

Mhariri
+255 789 201383

Tutafakari haya tunaposherehekea Idd el-Fitri

Waislamu duniani kote hivi sasa wapo katika shamrashamra za Sikukuu ya Idd el-Fitri baada ya kukamilika mwezi Mtukufu wa Ramadhan.

Mwezi wa Ramadhan ni darasa la kutoa mafunzo ya umoja, huruma, mshikamano, kupambana na maradhi ya chuki, fitina na uhasama, ambayo Waislamu wengi wanaugua.

Licha ya idadi kubwa ya Waislamu wanaofunga mwezi wa Ramadhan, bado malengo tarajiwa ya Ramadhan hayafikiwi katika mkakati wa kutafuta suluhu ya changamoto za Waislamu.

Hali hii inatokana na baadhi yetu kutofahamu falsafa na malengo ya swaumu ya Ramadhan. Ukweli wa suala hili unathibiti katika hadith ya Mtume (Allah amshushie rehema na amani) isemayo: "Uislamu ulianza ukiwa mgeni na utaondoka ukiwa ni mgeni kama ulivyoanza..." [Muslim].

Kutofahamika vema chimbuko la madhehebu ya Kiislamu, misingi, itikadi na fikra za wafuasi wake, pia kunatajwa kuwa chanzo cha baadhi ya Waislamu kuchukiana na kuhasimiana. Kwa kuzingatia mustakbali na maslahi mapana ya umma, si jambo la busara kwa Waislamu kufarakana, kuchukiana na kusemana vibaya kwa sababu ya tofauti ndogondogo.

Mola wetu Mtukufu anatuambia: "Hapana kulazimisha katika dini, kwani uongofu umekwishapambanuka na upotofu..." [Qur'an, 2:256]. Hakuna asiyejua kuwa, kuunga undugu na umoja ndiko kunakopelekea watu kupendana, kujuliana hali, kunasihiana, kuombeana dua kwa Allah, kufanyiana wema na uadilifu, kusaidiana na kusameheana.

Waislamu wa Tanzania wanaweza kuwa mfano wa kuigwa katika hili. Ni jambo linalofahamika na wengi kuwa dhana ya umoja na utangamano kwa Waislamu hapa nchini huchipua mizizi wakati wa mwezi Mtukufu wa Ramadhan, kadhalika unapowadia msimu wa safari za Hijja.

Kwa nini tuwe wamoja?

Tunapoitazama Qur'an Tukufu na Sunna za Mtume (rehema na amani ya Allah iwe juu yake), tunabaini kuwa viwili hivyo vimetilia mkazo suala la umoja na utangamano baina ya Waislamu. Hii inatokana na faida nyingi za umoja na utangamano, ikiwamo kudumisha amani, utulivu na usalama, kustawi kwa uchumi, na kuwa mbali na machafuko, vita na umwagaji wa damu.

Historia ya Uislamu inatuarifu kuwa moja ya fikra asilia za Mtume (Allah amshushie rehema na amani) ilikuwa ni kuwauganisha Waislamu. Mtume aliondoa kila aina ya utata unaoweza kuwasha moto wa chuki na uhasama miongoni mwa jamii ya Waislamu, aliwaunganisha na kupandikiza mahaba kati yao kupitia muafaka wa undugu.

Katika kile kinachopaswa kupewa kipaumbele, ni Waislamu kuzingatia malengo na maslahi makuu ya dini huku wakijiepusha na kuchochea moto wa fitina na mifarakano isiyo na msingi.

Sote tunaelewa kuwa fitina ni moto wenye kuangamiza kikavu na kibichi, na pia ni silaha inayoweza kuangamiza umma.

Mfano halisi wa kadhia hii tunaupata katika mgogoro wa kihistoria kuhusiana na mwandamo wa mwezi Mtukufu wa Ramadhan, hali kadhalika utata wa tarehe au siku sahihi kwa Waislamu kufunga swaumu ya Arafa.

Kwa kuzingatia athari zitokanazo na tofauti hizi, wakati umefika wa kuchukua maamuzi ya pamoja kwa lengo la kudhamini maslahi ya pamoja ya Waislamu. Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema: "Hakika waumini (wote) ni ndugu, basi patanisheni baina ya ndugu zenu. Na mcheni Allah ili mpate kurehemewa." [Qur'an, 49:10].

Sanjari na hilo, wasomi na wanazuoni wetu wana jukumu la kuwanasihi Waislamu kujiepusha na masuala yanayozusha utata miongoni mwao. Jamii yetu inapaswa kuyatekeleza haya kivitendo ili kujinasua na changamoto hizi.

Tunafahamu wapo baadhi yetu wanaotamani kuona siku moja Waislamu wanaishi katika hali ya umoja, lakini ni vigumu jambo hilo kutekelezeka kwani tulio wengi hatuko tayari kuheshimu mitazamo ya kiitikadi na kifiqhi ya watu wengine.



MAKALA MAALUM

NA ZAHARANI BARAKA

Kuendeleza mema baada ya Ramadhan

Nuzuri ulioje mema kufuatiwa na mema. Hivyo ndivyo [illegible]liyotuelekeza Allah kwa faida [illegible] "M[illegible] wa[illegible]amb[illegible] la [illegible] N[illegible] ya[illegible]kia n[illegible] bora mbele ya Mola wako Mlezi kwa malipo, na bora kwa matumaini." [Qur'an, 18:46].

Kuna umuhimu mkubwa wa kuendeleza na kudumisha mema, kwani kama tulivyo na juhudi ya kutenda mema tunatakiwa tuwe na hima ya kutaka matendo yetu yakubaliwe na Allah.

Allah Aliyetukuka ameweka wazi kuwa huwakubalia wachamungu. Na mtu hawezi kuwa mchaji ila awe ni mwenye kudumisha ibada. Kama ilivyo kwa mema kuwa yanaondosha maovu, basi tujue kuwa maovu yanaharibu mema.

Kudumisha mema hupelekea makosa madogo madogo kusamehewa. Allah anasema: "Na shika sala katika ncha mbili za mchana na nyakati za usiku zilizo karibu na mchana. Hakika mema huondoa maovu. Huu ni ukumbusho kwa wanaokumbuka." [Quran, 11:114].

Pia, kuendeleza maovu ni sababu kubwa ya kuharibu mema, ambayo tumeyafanya katika mwezi mtukufu wa Ramadhan. Siku, miezi, na miaka – vyote vimekadiriwa muda maalumu na ndiyo nyakati za matendo. Na matendo humalizika kwa kumalizika nyakati. Nyakati hizo ndiyo chombo cha matendo yetu.

Hii ina maana tutakwenda kuulizwa mbele ya Allah juu ya matendo tuliyoyafanya siku fulani au mwezi fulani au mwaka fulani. Allah anasema katika hadithil Qudsy: "Enyi waja wangu! Hayo ni matendo yenu, ninayadhibiti kisha nitakutimizieni malipo yake. Atakayekuta kheri amshukuru Allah; na atakayekuta kinyume na hivyo asila[illegible] ila nafsi yake." [Muslim].

M[illegible]ezi w[illegible] R[illegible] u[illegible]ne-ondoka na matendo yetu tuliyoyafanya ndani yake. Aliyefanya mema adumishe mwenendo huo na aliyekosea arejee kwa Mola wake kwani fursa bado ipo.

Ulikuwa mwezi mwema, watu walikuwa wema wakifunga mchana wake na kusimama usiku wake pamoja na kujikurubisha kwa Allah kwa aina mbalimbali za matendo mema, kwa matumaini ya kupata radhi za Allah na kwa kuogopa adhabu yake.

Muislamu anatakiwa kuishi baina ya hofu na matumaini, akihofia adhabu ya Allah huku akitumai thawabu zake zitakazopelekea kupata hali nzuri ya raha na furaha mbele ya Allah.

Hata hivyo, thawabu zinaambatana na juhudi ya mtu katika twa'a za aina mbalimbali katika nyakati zote, miezi yote na siku zote – si katika Ramadhan tu.

Kuna wengi waliotarajia kuwemo ndani ya Ramadhan lakini hawakuwezeshwa. Ajali zao ziliwakuta kabla ya kuingia Ramadhan. Kuna walioingia lakini hawakupata nafasi ya kufanya heri nyingi ndani ya mwezi huu, kwani hawakuumaliza. Na kuna walioudiriki lakini hawakufanya chochote.

Kwa sisi ambao Allah ametuwezesha kufanya mema ndani ya Ramadhan tumebaki na matumaini, hivyo hatupaswi kuchafua juhudi ndogo tuliyoifanya baada ya mwezi huu.

Kupata faida ndani ya Ramadhan kuna alama zake, na kupata hasara kuna alama zake. Aliyefaidika na mwezi wa Ramadhan utamuona akidumu na kuendeleza utii wake kwa Allah; na aliyepata hasara utamuona akiangukia katika dimbwi la maasi baada ya Ramadhan na kughafilika na mambo mengi ambayo ni wajibu kwake.

Msimu wa Ramadhan umemalizika ila ibada bado zipo pale pale. Kama ni kufunga, bado funga za sunna zipo mwaka mzima, hivyo basi tunatakiwa tudumishe ibada ya funga. Baada ya Ramadhan tunaanza na sunna ya siku sita za mwezi wa Shawwal ili tupate fadhila za funga ya mwaka mzima.

Kama ni kisimamo cha usiku ni jambo linalotakiwa kuwa endelevu. Allah huteremka hadi katika uwingu wa dunia kila siku inapobaki theluthi ya mwisho ya usiku kwa ajili ya kutoa msamaha kwa wanaoomba msamaha na kuwapa wanaoomba mahitaji yao. Tutumie fursa hii inayopatikana kila siku wala si katika Ramadhan tu.

Kusoma Qur'an ni jambo muhimu kwa Muislamu wakati wote. Kikubwa tutambue kuwa Ibada ni sehemu katika maisha ya mwanadamu na si katika muda fulani tu. Matendo bora ni yale ya

شوّال

NASAHA ZA WIKI

0787 503 085

NA YUSUFU AMINI

Mwanao amejifunza haya ndani ya Ramadhan?

Hivi umejiuliza watoto wako wamejifunza nini katika Ramadhan ya mwaka huu? Ni kweli watu wazima ndiyo waliofaradhishwa kufunga mwezi wa Ramadhan, lakini kwa upande mwingine watoto wanatakiwa kuutumia mwezi huo kujifunza ibada, nidhamu na maadili ya dini. Hivyo, yaweza kusemwa kuwa mwezi wa Ramadhan ni shule ya kiroho na kimaadili kwa watoto.

Ramadhan humfundisha mtoto nidhamu – si tu katika kula na kunywa, bali pia katika maisha yake ya kila siku. Ndani ya Ramadhan, watoto hujitahidi kufunga, kusali kwa wakati na kushiriki mambo mbalimbali ya kiibada.

Qur'an tukufu inasisitiza nidhamu hii na utii: "Enyi mliyoamini! Mmelazimishwa kufunga kama walivyolazimishwa waliokuwa kabla yenu ili muwe wachamungu." [Qur'an, 2:183]. Aya hii inatufundisha kwamba swaumu ya Ramadhan si adhabu kwa wakubwa wala watoto, bali ni njia ya kujenga uchamungu na utulivu wa nafsi.

Ibada na ukarimu

Watoto hujifunza kuwa na huruma kwa masikini na wenye uhitaji. Kupitia funga, wanahisi njaa na kiu na hivyo kuelewa hali ya wale wasiopata chakula kila siku. Mtume (Allah amshushie rehema na amani) amesema: "Si muumini yule anayeshiba hali ya kuwa jirani yake ana njaa." [Bukhari].

Katika mwezi wa Ramadhan, watoto huwa karibu zaidi na Mwenyezi Mungu kupitia sala, usomaji wa Qur'an na dhikri. Kupitia sala za faradhi na sunna (ikiwamo tarawehe), na kupitia mashindano mbalimbali ya kusoma na kuhifadhi Qur'an, watoto huelewa thamani ya Qur'an, ibada ya sala na nyinginezo.

Mtume amesema: "Wafundisheni watoto wenu kusali wakiwa na miaka saba, na wapigeni wakiacha sala wanapofikisha miaka kumi." [Sunan Abu Daudi]. Kuna faida nyingi za kuwafundisha na kuwahimiza watoto kusali sala za faradhi msikitini na zile za sunna. Miongoni mwa faida hizo ni kujitoa kwenye dhima mbele ya Mwenyezi Mungu na kutaraji malipo ya kuwazoesha watoto kufanya ibada.

Kuhusu hilo, Mtume wa Allah (rehema na amani imshukie) amesema: "Mwenye kulingania (kuhubiri) uongofu atapata katika malipo mfano wa malipo ya watakaomfuata. Hilo halipunguzi chochote katika malipo yao (hao waliomfuata)." [Muslim].

Faida nyingine ni kwamba, mtoto anayesali anakua katika ulinzi wa Allah na uchungaji wake siku nzima, kwa kauli ya Mtume (rehema za Allah na amani imshukie) aliposema: "Yeyote anayesali Alfajiri katika jamaa, basi yumo katika dhima (hifadhi) ya Mwenyezi Mungu." [Ibn Majah].

Faida nyingine ni kumtoa mtoto katika kundi la makafiri na wanafiki atakapokuwa mkubwa, kama alivyosema Mtume: "Tofauti iliyopo baina yetu (Waislamu) na wao (makafiri) ni sala. Kwa hiyo, mwenye kuacha sala amekufuru." [Ahmad].

Subira na shukrani

Mwezi wa Ramadhan huwafundisha watoto uvumilivu na kushukuru kwa kule kuacha kwao kula na kunywa katika mchana wa Ramadhan. Hali hii huwajenga kitabia na kisaikolojia, wakielewa kuwa dunia ni mahali pa mtihani na majaribu, na kwamba thawabu na malipo makubwa hutokana na subira na uvumilivu.

Subira ndani ya mwezi wa Ramadhan hudhihiri katika kudhibiti hasira, kuacha kusema uongo na kuepuka magomvi – tabia ambazo mtoto anatakiwa kuzidhibiti katika miezi mingine.

Kujiamini na uwajibikaji

Waislamu duniani kote hutekeleza swaumu ya Ramadhan kwa wakati mmoja, jambo ambalo humjengea mtoto hisia ya umma mmoja.

Mtoto anapofunga, hata kwa saa chache, au kusaidia kuandaa futari, humfanya kuwa na roho ya utu na uwajibikaji katika maisha ya baadaye.

Mtoto anapofunga, japo kwa saa chache, huhisi machungu ya kiu na njaa wanayopitia watu wengine, hivyo ni rahisi kwake kukumbuka na kuelewa uhalisia wa binadamu wenzake wanaoishi katika lindi la umasikini.

Mtoto aliyezoea kula milo zaidi ya mitatu kwa siku, iwapo atashinda na njaa kutwa nzima, hata kwa siku chache za Ramadhan, itakuwa rahisi kwake kuelewa uhalisia wa maisha ya masikini na mafukara.

Kimsingi, mwezi wa Ramadhan ni chuo cha malezi kwa watoto, kinachowafunza nidhamu, subira, huruma, ibada na umoja. Watoto wanaojishughulisha na mambo mema ndani ya Ramadhan huendeleza sifa hiyo hata baada ya mwezi huo kuisha.

شَوَّال

KALAMU HURU

SEHEMU YA 1

SHEIKH
Shaaban Mussa
0786 272 323

Uchamungu (Taqwa) - tunda kuu la Ramadhan

Mwezi wa Ramadhan ulikuwa ni zaidi ya kujizuia kula na kunywa; ni shule kamili ya malezi ya nafsi iliyomlea Muislamu kufikia daraja la juu kabisa la kiroho; daraja la uchamungu (taqwa) na ndio maana Allah Mtukufu alipofaradhisha funga, hakuishia tu kusema "fungeni", bali alibainisha lengo kuu la ibada hiyo pale aliposema: "Ili mpate kumcha Mungu." [Qur'an, 2:183].

Kutokana na ukweli huo, swali la msingi ni je uchamungu ni nini? Na je, tunapaswa kuubeba vipi baada ya Ramadhan kuisha? Uchamungu (taqwa) ni hali ya moyo inayomfanya mja awe na uangalifu wa hali ya juu mbele ya Mwenyezi Mungu katika kila jambo analolifanya.

Zaidi, uchamungu ni kujenga kizuizi baina yako na adhabu ya Allah kwa kutekeleza amri zake na kujiepusha na makatazo yake. Kwa maneno mengine, ni kuishi maisha ya utii kwa Allah kwa siri na kwa dhahiri.

Katika mwezi wa Ramadhan, Muislamu huanza kujizoeza uchamungu kwa njia ya kipekee sana. Anajizuia kula na kunywa si kwa sababu hakuna chakula, bali kwa sababu anajua kuwa Allah anamuona. Angeweza kunywa maji akiwa peke yake na hakuna anayemuona, lakini anachagua kujizuia. Hapa ndipo kiini cha taqwa kinapoanza kujengeka: hisia ya kuwa Allah yupo pamoja nawe kila wakati.

Hii ndiyo tofauti kubwa kati ya funga na ibada nyingine. Ibada nyingi zinaonekana kwa watu, lakini funga ni siri kati ya mja na Mola wake. Hivyo, funga inamfundisha Muislamu kuwa mwaminifu kwa Allah hata pale ambapo hakuna mwanadamu anayemuangalia.

Hata hivyo, uchamungu wa Ramadhan hauishii kwenye chakula na vinywaji pekee bali kujizuia na mambo mengine mabaya kama vile kusema uongo, kusengenya, kuangalia haramu, na kufanya dhuluma. Hii ina maana kwamba Ramadhan ni mafunzo ya kujidhibiti kwa kiwango cha juu zaidi si kwa tumbo tu, bali kwa ulimi, macho, masikio, na moyo. Swali la kujiuliza baada ya Ramadhan ni je, mafunzo haya yanaishia mwezi wa Ramadhan tu?

Kwa bahati mbaya, baadhi ya Waislamu huonesha mabadiliko makubwa ndani ya Ramadhan; wanatoa sana sadaka, zaka, wanaswali, wanasoma Qur'an, na wanajiepusha na maasi, lakini mara tu mwezi unapomalizika, hurudi katika hali yao ya zamani. Hii inaashiria kwamba lengo la funga halikufikiwa ipasavyo.

Uchamungu wa kweli si wa msimu; ni mtindo wa maisha. Ramadhan inapaswa kuwa mwanzo wa safari mpya, si mwisho wa ibada. Ikiwa mtu amezoea kuswali kwa wakati ndani ya Ramadhan, basi anapaswa kuendelea hivyo hata baada ya Ramadhan. Ikiwa ameacha maasi, basi asiyaendee tena.

Miongoni mwa njia za kudumisha uchamungu baada ya Ramadhan ni kuendelea na ibada za hiari kama vile kufunga Sunna, kusoma Qur'an kila siku, na kufanya dhikri. Pia ni muhimu kujichunga na mazingira yanayoweza kumrudisha mtu katika maasi, kama vile marafiki wabaya au matumizi mabaya ya mitandao.

Vilevile, ni muhimu kwa Muislamu kujikumbusha kila mara kwamba Allah humuangalia wakati wote, si katika Ramadhan tu. Hii itamsaidia kubaki katika mstari wa uchamungu, hata anapokuwa peke yake. Kujenga tabia ya kujitathmini (muhasaba) kila siku pia ni silaha muhimu ya kudumisha taqwa.

Nihitimishe kwa kusema aliyefanikiwa si yule aliyefunga Ramadhan pekee, bali ni yule ambaye Ramadhan imembadilisha na kuendelea kubeba mabadiliko hayo katika maisha yake yote. Hivyo basi, Ramadhan iwe ni mwanzo wa maisha mapya yenye uchamungu, utii, na ukaribu wa kweli kwa Mwenyezi Mungu.

Lakini uchamungu hauwezi kusimama peke yake bila nguzo muhimu inayoubeba; nayo ni subira. Ndani ya Ramadhan, Muislamu amejifunza kuvumilia njaa, kiu, na matamanio yake; lakini je, anaendeleaje na subira hiyo baada ya Ramadhan?

Katika makala inayofuata, tutazungumzia kwa kina kuhusu subira kama moja ya mafunzo makubwa ya Ramadhan, na jinsi ya kuendelea nayo katika maisha ya kila siku.

MAKALA MAALUM

SHEIKH
Seif Ruga
0712 690 811



Kuzuru makaburi kunakoruhusiwa kisharia

Mwanzoni mwa Uislamu, suala la kuzuru makaburi lilikuwa limekatazwa, lakini baadaye likaruhusiwa na kuwekewa masharti maalum. Shekhul Islami Ibn Taymiyya (Allah amrehemu) amenukuu sababu zilizotajwa kuhusu kukatazwa kuzuru makaburi katika miaka ya mwanzo ya Uislamu.

Kuzuru makaburi kunakoruhusiwa kisharia

Mwanzoni mwa Uislamu, suala la kuzuru makaburi lilikuwa limekatazwa, lakini baadaye likaruhusiwa na kuwekewa masharti maalum. Shekhul Islami Ibn Taymiyya (Allah amrehemu) amenukuu sababu zilizotajwa kuhusu kukatazwa kuzuru makaburi katika miaka ya mwanzo ya Uislamu.

Ibn Taymiyya alisema: "Imesemwa kuwa kukatazwa huko kulitokana na kuhofia kuingia kwenye vitendo vya ushirikina. Wengine wamesema ni kwa sababu ya maombolezo yasiyofaa yaliyokuwa yakifanywa makaburini. Na wengine wamesema ilikatazwa kwa sababu ya watu kujivuna (kujifaharisha) katika makaburi ya wafu waliotangulia."

Kwa upande wake, Sheikh Albani (Allah amrehemu) amesema kuwa katazo hilo lilikuwa mwanzoni mwa Uislamu katika mji wa Makka. Tunathibitisha hili kwa yakini japokuwa hatuna tarehe kamili ya kihistoria, lakini mantiki sahihi inaunga mkono jambo hili.

Kauli ya Mtume wa Allah (rehema na amani zimshukie): "Nilikuwa nimewakataza kuzuru makaburi, sasa yazuruni," haikuwa katika mji wa Madina. Katika mji wa Makka, hukumu nyingi zilihusu mambo ya itikadi na kumpwekesha Allah (Tauhid), na katazo la kuzuru makaburi lililenga kufunga milango ya ushirikina.

Katika zama za mwanzo za Uislamu ambapo watu wengi walikuwa na kumbukumbu za vitendo vya ushirikina, Mtume aliwakataza kuzuru makaburi ili wasije kurudi kwenye ushirikina.

Imani na itikadi yao ilipoimarika katika kumpwekesha Allah, ndipo Mtume akawaruhusu kuzuru makaburi. Hivyo, tuna yakini kwamba katazo lilikuwa katika mji wa Makka na siyo Madina.

Wanazuoni wote wa umma wamekubaliana kuwa kuzuru makaburi ni sunna kwa wanaume, na wametofautiana kwa upande wa wanawake. Hairuhusiwi kisharia kuandaa safari mahsusi kwa ajili ya kuzuru makaburi pekee. Inasikitisha kuona kuwa watu wengi katika zama zetu hizi hawajui sharia za kuzuru makaburi.

Wengi wao huenda makaburini wakati ndugu au marafiki zao wanapofariki. Na miongoni mwa wale wenye desturi ya kuzuru makaburi, hawafanyi hivyo kwa lengo la kujifunza, kuwaidhika, kukumbuka Akhera wala kuwaombea dua marehemu.

Kwa upande mwingine, kuna watu wanaopitiliza katika utekelezaji wa ibada hii kwa kuyazuru makaburi mara nyingi kupita kiasi, ambapo karibu ibada zao zote na njia zao za kujikurubisha kwa Allah hutegemea ziara za makaburi ya masharifu, mawalii, watu wema, wakuu wa familia na wazee wa kimila.

Baadhi yao wamefikia hatua ya kuamini kuwa wafu hao wana uwezo wa kuleta jambo jema au kuzuia madhara, hivyo huwaomba wapate kazi, watoto, mali na kadhalika. Kwa njia hii hujikuta wameangukia katika dhambi ya shirk.

Kuzuru makaburi ni lazima kuendane na mafundisho ya Mtume wa Allah (rehema na amani zimshukie) kwa umma wake, ikiwamo kuwasalimia waliolala humo na kuwaombea dua ya rehema na msamaha.

Kuzuru makaburi kunafanana kimaana na sala ya jeneza, kwani anayesalia jeneza humkusudia marehemu kwa dua ya rehema. Kwa hiyo, anayezuru makaburi akusudie kuwaombea dua wafu kwa njia iliyoidhinishwa na sharia ili apate thawabu zilizoahidiwa.

Miongoni mwa dua mashuhuri aliyoelekeza Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) isomwe wakati wa kuzuru makaburi ni ile inayosema: "Assalamu alaykum ahladdiyaari minal mu'minina wal-muslimiin, wa innaa in shaa Allahu bikum laahiqun, nas'alullaaha lanaa wa lakumul aafiyah."

Maana yake: "Amani iwashukie enyi wakaazi wa nyumba hizi miongoni mwa waumini na Waislamu. Na kwa hakika sisi, kwa idhini ya Allah tutakutana nanyi. Tunamuomba Allah atupe sisi na ninyi salama na afya."

Hekima ya kuzuru makaburi

Miongoni mwa hekima ya ibada ya kuzuru makaburi ni kukumbuka mwisho wa uhai. Hili limeelezwa katika hadith ya Mtume isemayo: "Anayetaka kuzuru makaburi ayazuru, kwani (huko kuzuru makaburi) kutawakumbusha kifo."

Kuzuru makaburi ni njia ya kupata thawabu na malipo kutoka kwa Allah ikiwa ibada hiyo itafanywa kwa nia njema na ikhlas. Pia, kuzuru makaburi huwanufaisha maiti kwa kuwatolea salamu, kuwaombea dua na msamaha. Mtume wa Allah alikuwa akiyazuru makaburi ya Masahaba zake ili kuwaombea rehema na msamaha. Huu ndiyo mfumo aliouweka Mtume kwa umma wake.

Kumzuru Mtume Madina

Inapaswa kufahamika kwamba mtu anaposafiri kwenda Madina kisha akasali katika msikiti wa Mtume, ni sunna iliyokubaliwa na wanazuoni wote kulizuru kaburi la Mtume wa Allah. Mwanazuoni Qadhi Iyadh amesema: "Baadhi ya watu walinieleza kuwa walimwona Imam Malik bin Anas akija kwenye kaburi la Mtume, anainua mikono yake kiasi kwamba walidhani ameanza kusali, kisha anamtolea salamu Mtume na kuondoka."

Imam Malik hakuwa akipendekeza kufanya chochote katika kaburi la Mtume isipokuwa kutoa salamu tu. Naye Sheikhul Islami Ibn Taymiyya (Allah amrehemu) amesema kuwa Imam Malik alikuwa miongoni mwa wanaojua zaidi jambo hili, kwa kuwa aliwaona Taabiina ambao nao waliwaona Masahaba wa Madina.

Kwa sababu hiyo, Imam Malik alikuwa akipendekeza kufuata mwenendo wa waliotangulia, na alichukia mtu kubuni jambo jipya kwenye kaburi la Mtume. Imam Malik aliwachukia wale wanaosimama muda mrefu au kuomba dua kwenye kaburi la Mtume, kwa kuwa Masahaba hawakufanya hivyo.

"Afya" is natural source of sweet drinking water from underground stream which is blended with essential minerals to support and aid perfect metabolism.

WATERCOM LIMITED

P.o. Box 20409, Plot N.4005, Kisarawe11 area Temeke, Dar es Salaam, Tanzania. www.watercomtz.com, Email:info@watercomtz.com

شَوّال

TUJIFUNZE AI (ARTIFICIAL INTELLIGENCE)

Na Junaynat Ally Dama



Je, tuache watoto watumie akili mnemba au la?

Wiki hii katika safu hii inayohusu akili mnemba (Artificial Intelligence – AI) tunajadili swali linalowasumbua wazazi na walimu wengi: je, watoto wanapaswa kuachwa kutumia teknolojia hii katika masomo yao au la?

Kadiri AI inavyozidi kuingia katika maisha ya kila siku, watoto nao wameanza kuitumia mapema. Tafiti na uchunguzi mbalimbali zinaonesha kuwa hata watoto wenye umri wa chini ya miaka 10 tayari wanajaribu zana za akili mnemba katika kufanya kazi za shule au kujifunza mambo mapya. Hali hii imeibua mjadala mkubwa kuhusu athari zake kwa elimu na maendeleo ya watoto.

Kwa ufupi, akili mnemba ni teknolojia inayowezesha kompyuta kufanya kazi ambazo hapo awali zilihitaji akili ya binadamu. Kupitia mbinu kama 'machine learning', kompyuta hujifunza kutoka katika kiasi kikubwa cha taarifa na kisha kutumia maarifa hayo kujibu maswali, kuelewa lugha, kutambua picha au hata kuandika maandishi.

Ndiyo maana zana kama ChatGPT zimekuwa maarufu sana tangu zilipoanza kutumika kwa umma mwaka 2022. Mfumo huu unaweza kufanya mazungumzo ya kawaida na mtumiaji, kujibu maswali na hata kutengeneza maudhui kama hadithi, mashairi au nyimbo. Kwa wanafunzi, uwezo huo unaweza kuwa msaada mkubwa katika kujifunza.

Katika mazingira ya shule, AI inaweza kusaidia kwa njia nyingi. Wanafunzi wanaweza kuitumia kufanya utafiti wa awali, kutafsiri lugha, kuelewa dhana ngumu, kupanga muundo wa insha, kusahihisha tahajia au hata kupata maswali ya kujipima kabla ya mtihani. Pia kuna zana zinazoweza kubadilisha maandishi kuwa sauti kwa wanafunzi wasioona vizuri au kubadilisha sauti kuwa maandishi kwa wanafunzi wenye changamoto ya kusikia.

Lakini pamoja na uwezo huo, wasiwasi wa wazazi na walimu unaendelea kuwepo. Hoja kubwa ni kwamba watoto wanaweza kutegemea sana AI na kupunguza uwezo wao wa kufikiri kwa kina.

Kazi za nyumbani kwa kawaida hutolewa ili kuwasaidia wanafunzi kuimarisha uelewa, kukuza uwezo wa kuchambua na kufanya mazoezi ya kutatua matatizo. Ikiwa teknolojia itafanya kazi hiyo yote, mwanafunzi anaweza kukosa fursa muhimu ya kujifunza.

Changamoto nyingine ni suala la udanganyifu wa kitaaluma. Ikiwa mwanafunzi atatumia AI kuandika insha nzima au kujibu maswali na kisha kuwasilisha kazi hiyo kama yake bila kutaja msaada wa teknolojia, hilo linachukuliwa kama wizi wa kazi za kitaaluma.

Hii ndio sababu baadhi ya shule awali zilipiga marufuku matumizi ya zana kama ChatGPT, ingawa taasisi nyingi sasa zimeanza kuruhusu matumizi yake kwa masharti maalum.

Aidha, kuna tatizo la usahihi wa taarifa. Wataalamu wa teknolojia wanakiri kuwa wakati mwingine AI inaweza kutoa majibu yanayosikika kuwa sahihi lakini yakawa na makosa au yamepitwa na wakati.

Sababu ni kwamba mifumo hii hutumia takwimu na data ilizofundishwa, badala ya kuelewa mambo kwa mantiki kama binadamu. Hivyo mwanafunzi anapaswa kujifunza kuthibitisha taarifa kutoka katika vyanzo vingine vinavyoaminika.

Kwa mtazamo mpana, wataalamu wa elimu wanasema tatizo si matumizi ya akili mnemba yenyewe bali namna inavyotumiwa. Ikiwa itatumika kama nyenzo ya kusaidia kujifunza—kwa mfano kuelewa dhana kabla ya kujaribu kuitatua mwenyewe—inaweza kuongeza ubunifu na kuchochea udadisi wa mwanafunzi.

Kwa hiyo, badala ya kuuliza kama watoto wanapaswa kutumia AI au la, swali sahihi zaidi ni: wanapaswa kuitumia vipi? Wazazi na walimu wanahimizwa kuweka kanuni rahisi za matumizi—kama kuitumia kwa utafiti wa awali, kuuliza maswali bora zaidi, na kuthibitisha majibu kutoka katika vyanzo vya kuaminika.

شَوَّال

MAKALA YA AFYA
0764 101 018

Kupanda BP nyakati za usiku, hatari nyingine kubwa iliyofichika!

Watu wengi hupima shinikizo la damu mchana au wanapojisikia vibaya, lakini utafiti wa 2024–2025 unaonyesha kwamba kupima usiku, ni muhimu zaidi kuliko nyakati za mchana.

Kwa kawaida, binadamu anaposinzia mwili wake unaingia katika mapumziko ambapo mabadiliko kadhaa hutokea.

Kwanza, moyo hupiga taratibu na kupunguza mapigo yake kufikia mapigo 60-70 kwa dakika; pili, misuli hutulia na kupunguza matumizi yake ya hewa ya oksijeni; tatum. mfumo wa neva hupunguza kasi; na nne BP hushuka kwa asilimia 10–20 hali inayoitwa kitaalamu kama "dipping pattern" ambayo ni kawaida na salama kiafya.

Lakini, kwa baadhi ya watu aidha BP haishuki au haishuki kwa kiasi kinachokusudiwa au hupanda zaidi nyakati hizo za usiku! Aina hii ya shinikizo la damu inaitwa kitaalamu, "Nocturnal Hypertension" (shinikizo la damu la usiku).

Shinikizo la damu la usiku ni miongoni mwa visababishi vikuu vya kiharusi; kushindwa kwa moyo kufanya kazi; mshtuko wa moyo na kuharibika kwa figo bila mtu kugundua.

Kwa nini ni muhimu kufahamu BP yako nyakati usiku?

Kipimo cha BP nyakati za usiku ni kipimo sahihi zaidi (reproducible), ni kiashiria madhubuti cha vifo vinavyohusiana na moyo na hutambua shinikizo la damu (BP) liliyojificha. (masked hypertension).

Kipimo cha BP nyakati za usiku pia hutambua magonjwa yaliyofichika (OSA) hali ya kushindwa kupumua nyakati za usiku, magonjwa ya figo, na kile kiitwacho 'autonomic neuropathy' (hali inayotokana na kuharibika kwa mishipa ya fahamu inayodhibiti kazi za mwili zisizo za hiari).

Takwimu za kisayansi (tafiti 2024–2025) zinasemaje?

Tafiti zinaonesha kuwa ongezeko la shinikizo la damu (BP) isiyo ya kawaida nyakati za usiku ni kati ya asilimia 35 hadi 60.

Kiwango hiki kimeonekana zaidi kwa baadhi ya makundi yafuatayo Waafrika, Waasia, wazee, watu wenye kusumbuliwa na maradhi ya figo na kisukari na watu wenye uzito mkubwa, wenye matatizo ya kupata usingizi (Sleep Apnea), na watumiaon chumvi kwa wingi (salt-sensitive).

Takwimu zaidi zinaonesha kuwa asilimia 40 ya wagonjwa huwa ni wenye shinikizo la damu (BP) la kawaida wanapokuwa ofisini kwa daktari lakini wanakuwa na shinikizo la damu (BP) isiyo ya kawaida nyakati za usiku.

Kadhalika, kwa mujibu wa takwimu, Shinikizo la damu (BP) nyakati za usiku huashiria uhatari wa maradhi ya moyo mara tatu hadi nne zaidi kuliko shinikizo la damu (BP) ya mchana hali ambayo ni muhimu sana kuifahamu.

Tafsiri ya miundo isiyo ya kawaida ya mabadiliko ya BP usiku.

Maadiliko ya miundo ya BP usiku ina tafsiri kadhaa kutegemea na aina ya mabadiliko yenyewe

Hali ya kwanza: Kushuka BP <10% (non-dipper)

Kushuka shinikizo la damu nyakati za usiku ni hali ya kawaida kwa watu wenye kusumbuliwa na maradhi ya figo, kisukari, na watu wenye umri mrefu (wazee) kuanzia miaka 65 na kuendelea.

Hali ya pili: kupanda BP (reverse-dipper)

Hii ni hali ya hatari zaidi kwa watu wengi na kwa bahati mbaya wengi wao hawajitambui. Watu wenye hali hupata kizunguzungu; na huenda ikasababisha vifo vya ghafla nyakati za usiku au kiharusi.

Hali ya tatu: kushuka sana BP (extreme dipper)

Kushuka kwa BP nyakati za usiku kwa kiwango zaidi ya asilimia 20 (>20%) huongeza hatari ya ubongo kukosa damu ya kutosha (ischemia) hasa kwa wazee. Kadhalika, husabibisha kizunguzungu; kuanguka mara kwa mara nyakati za usiku na wakati mwingine kiharusi.

Hali ya nne: Wastani mzuri wa BP mchana na kupanda usiku (BP ≥120/70 mmHg), bila kugundulika

Hali hii, ya watu kupata namba nzuri ya shinikizo la damu mchana na kupanda nyakati za usiku (BP ≥120/70 mmHg) bila kugundulika! (Isolated nocturnal hypertension) nayo ni hatari kwani husababisha mtu kupatwa na kiharusi nyakati za usiku.

DKT.
Omar A. Kasuwi
Daktari Bingwa Mshauri wa magonjwa Moyo!
Hospitali ya Chuo Kikuu cha Sokoine (SUA)

MATUKIO YENYE MAZINGATIO

NA ZAHARANI BARAKA

Mtu mmoja alimwendea Imam Malik bin Anas (Allah amrehemu) akamuuliza: "Ewe Abu Abdillah, nianzie wapi kuhirimia (Hijja)?" Imam Malik akasema: "Kutoka Dhul–Hulayfah, pale alipoanzia kuhirimia Mtume (rehema na amani zimshukie)." Yule mtu akasema: "Mimi nataka nianzie ihram msikitini."
Imam Malik akasema: "Usifanye hivyo." Yule mtu akasema: "Nataka nianzie msikitini karibu na kaburi (la Mtume)." Imam Malik akasema: "Usifanye hivyo, kwani naogopa usijepatwa na fitina." Yule mtu akauliza: "Fitina gani hiyo? Si maili chache tu naongeza!"
Imam Malik akamwambia: "Ni fitina gani iliyo kubwa zaidi kuliko kuona kwamba wewe umetangulia kupata fadhila ambayo Mtume (rehema na amani zimshukie) hakuitenda?!"
Kisha akasema: "Allah 'Azza Wajallah' amesema: 'Basi wajihadhari wale wanaopingana na amri yake isije ikawapata fitina, au ikawapata adhabu iumizayo." [Rejea kitabu 'Al–hilya' cha Abu Nuaym na 'Al–I'tiswam' cha Ashaatwibiy].

Mafundisho ya tukio

Hakika asili katika ibada ni kuzuiliwa, kwa maana haijuzu kuanzisha ibada mpya mpaka ithibitike kwa dalili sahihi ya kisharia inayofanyiwa kazi katika Kitabu na Sunna.

Kwa hiyo, ibada au tendo la kujikurubisha kwa Allah lisilo na msingi wa maandiko sahihi ya sharia ni uzushi (bid'a iliyokataliwa) na ni amali itakayorudishwa kwa mhusika, kama alivyosema Mtume (rehema na amani zimshukie): "Atakayezusha katika jambo letu hili (la dini) jambo lisilokuwepo, basi jambo hilo litarudishwa." [Bukhari na Muslim].

Sababu za kushamiri uzushi katika Ramadhan

Kwa msingi huo, imekuwa ni wajibu kwa watu wa elimu na dini kubainisha Sunna iliyofifia na kukemea bid'a na matamanio (hawaa) yanapodhihiri.

Bado tumo ndani ya mwezi Mtukufu wa Ramadhan, ambao tulio wengi tunajitahidi kujikurubisha kwa Allah kupitia ibada mbalimbali. Hata hivyo, siyo wote wanaofanikiwa kuyafikia malengo waliyojiwekea ndani ya Ramadhan.

Wapo wanaoshindwa kufikia malengo yao, si kwa sababu ya uvivu au kukosa ari, bali aina ya ibada wanazofanya hazina asili katika dini, na nyingine msingi wake unajulikana kisheria lakini wanaziharibu kwa namna wanavyozifanya.

Kanuni ya kisheria inasema: "Kuthibiti kwa jambo katika asili yake si hoja ya kuthibiti namna linavyofanyika (sifa yake). Inawezekana ibada ikawa inatambulika kisheria na ina dalili juu ya kuthibiti kwake lakini inavyofanywa ni kinyume na sheria." Hili ni tatizo kwa watu wengi na ni kikwazo kikubwa kwa sababu wanatazama asili tu.

Bid'a nyingi zimeenea katika nchi mbalimbali za Waislamu kwa sababu wanazuoni na wanafunzi wa elimu ya kisheria hawazikemei na kuzifafanua. Bid'a (uzushi) ni njia bunifu 'inayofanana' na sharia ikikusudiwa kuongeza bidii ya kujikurubisha kwa Allah, ilihali haina dalili sahihi ya kisheria.

Bid'a zote zimekatazwa na ni upotofu, kwa mujibu wa kauli ya Mtume (rehema za Allah amani zimshukie) aliposema: "Hakika mambo mabaya zaidi ni yale yaliyozushwa, na kila bid'a ni upotofu." [Ahmad na wengineo].

Miongoni mwa bid'a zinazofanywa kwa wingi ndani ya Ramadhan ni adhkaar mbalimbali zinazoimbwa misikitini baada ya sala huku baadhi yake zikiwa hazijathibiti kwa dalili sahihi.

Mfano wake ni adhkaar maalumu zinazosomwa katika sala ya tarawih baada ya salamu kila baada ya rakaa mbili, pamoja na dua ya nashid ya kuiaga Ramadhan inayosomwa kuanzia mwezi 15 na kuendelea. Hata adhkaar zilizothibiti kwa dalili sahihi nazo husomwa kwa sauti ya pamoja na mara nyingine huimbwa.

Mambo yote haya, ambayo mengine huondoa utulivu na unyenyekevu katika sala ya tarawih hayakuthibiti katika dini na wala wema waliotangulia hawakushikamana nayo. Watu hutumia muda mwingi kuimba nyiradi zisizothibiti katika sala ya tarawih badala ya kurefusha kisimamo kwa Qur'an.

Sababu za kuzuka na kuenea kwa bid'a

Kuna sababu nyingi zinazopelekea watu kufanya mambo ya uzushi, na miongoni mwa hizo ni ujinga wa kutoijua dini, kutothamini Sunna (mwenendo wa Mtume), kufuata matamanio ya nafsi, kuzungumzia dini pasina elimu, kutojua tofauti ya hadith sahihi na zisizo sahihi, na kufuata aya au dalili zenye utata bila kurejea katika uelewa wa wema waliopita (Salaf).

Baadhi ya wanazuoni hueneza ibada za bid'a kama njia ya kutafuta fedha au umaarufu. Hivi sasa mambo mengi ya bid'a yamegeuka kuwa desturi katika nchi zetu kiasi kwamba imekuwa vigumu kuziacha, hasa zinapolindwa na sheria au taratibu fulani katika nchi.

Athari za bid'a na njia ya kujikinga nazo

Mosi, bid'a inapoenea huchukua nafasi ya Sunna na kusababisha Sunna hiyo kufa na hatimaye kusahaulika kabisa. Pili, bid'a huleta mabishano yasiyo ya haki kwa sababu ya kutumika nguvu kubwa kuitetea.

Tatu, bid'a huchochea migogoro katika dini kwa sababu ya upinzani unaojitokeza kati ya wazushi na watetezi wa Sunna. Nne, bid'a huharibu uhusiano wa kidini na kuvuruga umoja wa Kiislamu. Tano, bid'a huwapoteza watu na kuwaweka mbali na njia ya haki.

Hakuna namna nyingine ya kujikinga na bid'a isipokuwa kufuata (kushikamana na) Kitabu cha Allah (Qur'an) na Sunna za Mtume (rehema na amani zimshukie) kwa uelewa wa wema waliopita, kueneza na kufundisha Sunna katika jamii ili kuondoa ujinga na kuwalinda watu dhidi ya bid'a, na kuamrisha mema na kukataza maovu kwa njia zilizo sahihi.

شوّال

MAKALA
MALEZI

JUNAYNAT ALLY DAMA

Ina maana gani mtoto wako balehe anapoanza kusema uongo?

Kwa wazazi wengi, kugundua kwamba mtoto wao wa balehe ameanza kusema uongo ni jambo linaloumiza na kusababisha wasiwasi.

Kwa mtazamo wa haraka, inaweza kuonekana kama ishara ya kutokuwa na maadili au kukosa heshima. Hata hivyo, wataalamu wa malezi na saikolojia ya vijana wanasema kuwa kusema uongo katika kipindi cha ujana mara nyingi ni sehemu ya kawaida ya ukuaji wa mtoto, si lazima iwe ishara ya uasi au tabia mbaya.

Kipindi cha ujana ni hatua ya mpito kati ya utoto na utu uzima. Wakati huu vijana wanajaribu kujitambua, kujenga uhuru wao na kujifunza namna ya kushughulikia mahusiano na wazazi pamoja na marafiki. Katika mchakato huu, kusema uongo kunaweza kujitokeza kwa sababu mbalimbali.

Mosi, hofu ya adhabu au kukataliwa

Sababu ya kawaida inayowafanya vijana kusema uongo ni hofu. Wanaweza kuogopa adhabu, kukosolewa au kupoteza uaminifu wa wazazi wao. Kwa sababu bado wanajifunza jinsi ya kukabiliana na matokeo ya matendo yao, wakati mwingine huona kusema uongo kama njia rahisi ya kuepuka matatizo.

Kwa mfano, kijana anaweza kusema uongo kuhusu alikokuwa au kazi ya shule ili kuepuka kukemewa. Hii haimaanishi lazima ana tabia mbaya, bali inaonyesha bado anajifunza jinsi ya kushughulikia makosa.

Pili, kutafuta uhuru

Ujana pia ni kipindi ambacho vijana wanataka kuwa na nafasi yao binafsi. Wanataka kufanya maamuzi yao na kujiona kama watu wanaojitegemea. Wakati mwingine, kusema uongo huwa njia ya kulinda uhuru huo.

Ikiwa kijana anahisi kuwa anadhibitiwa sana, anaweza kusema uongo ili kupata nafasi zaidi ya kufanya mambo yake bila kuingiliwa.

Tatu, kujenga taswira mbele ya wengine

Vijana pia hupitia kipindi cha kujitafuta—wanajaribu kuelewa wao ni nani na wanataka kuonekana vipi mbele ya watu wengine. Wakati mwingine wanaweza kusema uongo ili kuonekana bora mbele ya marafiki au kuepuka aibu.

Kwa mfano, kijana anaweza kusema ana alama nzuri zaidi shuleni au ana marafiki wengi zaidi ili kuimarisha taswira yakem asionekane kazubaa.

Nne, kujaribu mipaka ya wazazi

Katika hatua ya ukuaji wa akili, vijana huanza kupima mipaka waliyopewa. Wanaweza kusema uongo ili kuona wazazi watatikia vipi na kama sheria zilizowekwa zinafuatwa kwa uthabiti.

Hii, kwa mtazamo huo, huwa ni sehemu ya mchakato wa kujifunza kuhusu sheria, uwajibikaji na matokeo ya matendo.

Tano, kukosa ujuzi wa kuwasiliana

Wakati mwingine vijana husema uongo kwa sababu hawajui namna bora ya kueleza hisia zao. Wanaweza kuwa na aibu, hofu au msongo wa mawazo lakini hawana maneno ya kueleza hali hiyo.

Katika hali kama hiyo, kusema uongo huwa njia ya kuficha hisia au matatizo wanayopitia, wakiepuka suala la kujieleza kwa jambo hata wenyewe huwawia ngumu kuliwasilisha.

Wazazi wafanye nini?

Wataalamu wanashauri kwamba njia bora ya kushughulikia tatizo hili si hasira kali, bali mazungumzo ya wazi. Vijana huwa waaminifu zaidi wanapohisi kuwa wanaweza kusema ukweli bila kuogopa adhabu kali au kudhalilishwa.

Ni muhimu pia kuweka sheria zilizo wazi, juu ya misingi ya Uislamu, zinazotekelezwa kwa uthabiti ikiwemo kemeo kali dhidi ya uongo. Vijana wanahitaji kujua mipaka ipo, lakini pia wanahitaji kuhisi kuwa wazazi wanawaelewa.

Kwa ujumla, kusema uongo kwa vijana si jambo la kushangaza. Tafiti zinaonyesha kwamba idadi kubwa ya vijana huwahi kusema uongo kwa wazazi wao wakati fulani wa maisha yao. Hii haibadilishi uharamu wa kusema uongo.

Hivyo, badala ya kuona uongo kama usaliti mkubwa, wazazi wanaweza kuutazama kama ishara ya mchakato wa ukuaji. Kwa mawasiliano mazuri, uvumilivu na mifano ya uaminifu nyumbani, vijana wengi hujifunza polepole kwamba kusema ukweli hujenga uhusiano wa karibu na kuaminiana katika familia.

شوّال

MAKALA
SAIKOLOJIA

UKHTI FATIMA SS



Mambo 10 yanayopelekea kutopendwa na watu

Katika maisha ya kijamii na kikazi, mahusiano mazuri ni muhimu sana. Hata hivyo, kuna tabia fulani ambazo bila kujua zinaweza kuwafanya watu wakuepuke au kukosa kukuamini. Wataalamu wa saikolojia ya kijamii wamebainisha baadhi ya mienendo inayoweza kuharibu uhusiano kati ya mtu na watu wanaomzunguka.

Hapa chini ni mambo kumi yanayoweza kumfanya mtu asipendwe na wengine.

Mosi, kupenda kusengenya

Kusambaza maneno ya watu au kuzungumzia maisha ya wengine nyuma yao huondoa uaminifu. Watu wanaosengenya mara nyingi huonekana kama watu wasioweza kutunza siri. Matokeo yake ni kwamba watu huanza kujiepusha nao ili kulinda heshima na faragha zao.

Pili, kujali simu na kupuuza watu ulionao (Phubbing)

Neno phubbing linamaanisha kupuuza mtu aliye karibu kwa sababu ya kuangalia simu.

Unapokuwa kwenye mazungumzo lakini macho yako yako kwenye simu, ujumbe unaotumwa ni kwamba anayezungumza na wewe hana umuhimu. Tabia hii imekuwa chanzo kikubwa cha kukosekana kwa mawasiliano ya kweli katika zama za teknolojia.

Tatu, kulegea katika kazi za pamoja

Katika kazi za kikundi, baadhi ya watu hupunguza juhudi wakiamini kuwa wengine watafanya kazi kubwa. Tabia hii inayojulikana kama social loafing huwakatisha tamaa wenzako kwa sababu inaonekana kama kutokuwajibika.

Watu wanapogundua kuwa mtu hachangii ipasavyo, huwa wanapunguza imani kwake.

Nne, kujiona mtaalamu wa kila kitu

Kuna watu wanaamini kwamba wanajua kila jambo au wanajua kuliko wengine. Hali hii wakati mwingine huitwa expert fallacy.

Mtu anapokataa kusikiliza maoni ya wengine kwa sababu anaamini yeye ndiye mwenye maarifa zaidi, mara nyingi huonekana mwenye kiburi na mgumu kushirikiana naye.

Tano, kukana kosa hata ukiletewa ushahidi

Katika saikolojia, hali hii huitwa backfire effect. Ni pale mtu anaposhikilia msimamo wake hata baada ya kuonyeshwa ushahidi unaopingana na anachosema.

Badala ya kubadilisha mtazamo, mtu huyo hujilinda zaidi na kuendelea kusisitiza kuwa yeye yuko sahihi. Tabia hii huweza kuharibu majadiliano na kufanya watu wakose hamu ya kushirikiana.

Sita, kuhukumu watu haraka

Attribution bias hutokea pale mtu anapofanya hitimisho la haraka kuhusu tabia ya mtu mwingine bila kuzingatia mazingira. Kwa mfano, mtu akichelewa mara moja unaweza kudhani ni mzembe, bila kufikiria kwamba pengine kulikuwa na sababu nyingine. Tabia ya kuhukumu haraka inaweza kuharibu uhusiano kwa sababu inaonyesha ukosefu wa uelewa.

Saba, kuamini mafanikio ya wengine yanapunguza yako

Baadhi ya watu huamini kuwa maisha ni kama mashindano ambapo mafanikio ya mtu mmoja yanamaanisha hasara kwa mwingine.

Hii huitwa zero-sum fallacy. Mtazamo huu huzaa wivu na ushindani usio na afya, jambo linaloweza kuwafanya watu wakuepuke kushirikiana nawe.

Nane, kufikiria kila kitu kinahusu wewe

Self-referential bias ni tabia ya kutafsiri kila tukio kana kwamba linahusiana moja kwa moja na wewe. Kwa mfano, unaweza kudhani mtu amekukasirikia wakati pengine alikuwa na matatizo yake binafsi. Tabia hii inaweza kuleta migogoro isiyo ya lazima katika mahusiano.

Tisa, kujibu kabla ya kuelewa vizuri

Katika mazungumzo, watu wengine huanza kuandaa majibu yao kabla hata hawajamaliza kusikiliza. Hali hii huitwa response formulation bias. Matokeo yake hali hii kwamba mazungumzo yanakuwa ya juu juu kwa sababu mtu hasikilizi kwa makini bali anasubiri nafasi ya kujibu.

Kumi, kuwalaumu watu badala ya kuangalia mazingira

Fundamental attribution error ni pale tunapomlaumu mtu kwa tabia fulani bila kuzingatia mazingira yaliyomfanya afanye hivyo. Kwa mfano, unaweza kudhani mtu ni mvivu wakati pengine alikuwa na changamoto kubwa siku hiyo. Tabia ya kulaumu watu haraka huweza kuharibu mahusiano.

NA UKHTI FATIMA

Njia 8 za kuwa kiongozi bora

Watu wengi hudhani uongozi ni kipaji cha kuzaliwa nacho. Lakini tafiti nyingi za uongozi zinaonyesha kuwa uongozi ni zaidi ya tabia na stadi zinazojengwa kwa kujifunza na uzoefu.

Kwa maneno mengine, hakuna anayezaliwa akiwa kiongozi kamili; watu hujifunza kuwa viongozi kupitia maamuzi yao, mienendo yao na namna wanavyowahudumia wengine.

Hapa chini ni njia nane muhimu zinazoweza kumsaidia mtu kukuza uwezo wa uongozi katika maisha, kazini au katika jamii.

Mosi, chukua hatua

Moja ya sifa kuu za viongozi ni uwezo wa kuchukua hatua bila kusukumwa. Kiongozi haoni tatizo na kusubiri mtu mwingine afanye jambo; yeye hutambua hitaji na kuchukua hatua.

Hii inaweza kuwa kuanzisha mradi mpya, kutatua tatizo kazini au kusaidia timu inapokumbana na changamoto. Uongozi huanza pale mtu anapokuwa tayari kujitokeza na kuwajibika.

Pili, sikiliza kwa kujali

Kiongozi mzuri si yule anayezungumza sana bali anayejua kusikiliza. Kusikiliza kwa huruma kunamaanisha kujaribu kuelewa mawazo, hisia na mitazamo ya wengine.

Watu wanapohisi kuwa wanasikilizwa kwa dhati, hujenga uaminifu na hujihisi kuthaminiwa. Hii husaidia kujenga timu imara na maamuzi bora.

Tatu, jenga uaminifu

Uaminifu ni msingi wa uongozi. Watu hawafuati vyeo bali wanafuata watu wanaowaamini. Kiongozi anajenga uaminifu kwa kuwa mwaminifu, kutimiza ahadi na kuwa mtu wa kutegemewa.

Katika mazingira ya kazi au jamii, timu yenye uaminifu huwa na mshikamano zaidi na uwezo mkubwa wa kushirikiana.

Nne, onesha heshima

Kiongozi bora anathamini mchango wa kila mtu, bila kujali nafasi yake. Kuonyesha heshima kunamaanisha kusikiliza maoni ya wengine, kutambua juhudi zao na kuwaheshimu kama binadamu.

Mazingira ya heshima hujenga Imani, utii, mapenzi kwa kiongozi na utamaduni wa ushirikiano ambapo kila mtu anahisi ana nafasi na thamani ndani ya timu.

Tano, chatua hatua muda sahihi

Badala ya kusubiri matatizo yatokee, viongozi hujaribu kuyaona mapema na kutafuta suluhisho kabla hayajakuwa makubwa. Tabia hii huitwa kuwa "proactive."

Kiongozi anayefikiria mbele anaweza kupanga mikakati, kuandaa timu yake na kupunguza hatari zinazoweza kujitokeza.

Sita, toa mrejesho wa kweli kwa upole

Mrejesho ni sehemu muhimu ya maendeleo ya watu. Kiongozi mzuri husema ukweli lakini kwa namna inayojenga, si kuumiza. Mrejesho mzuri unakuwa wazi, wa heshima na wenye lengo la kusaidia mtu kuboresha utendaji wake. Badala ya kukosoa kwa hasira, kiongozi hutoa ushauri unaosaidia ukuaji.

Saba, uongozi si kufanya kila kitu mwenyewe bali kuwawezesha wengine kufanya vizuri.

Kiongozi anayewainua wengine huwapa nafasi ya kujifunza, kuwapa majukumu na kuwaamini katika kazi zao. Jambo hili huongeza uwezo wa timu na kuwafanya watu wajisikie sehemu muhimu ya mafanikio ya pamoja.

Nane, kuwa mfano

Hatimaye, uongozi ni mfano wa vitendo. Watu hujifunza zaidi kwa kuangalia matendo ya kiongozi kuliko kusikia maneno yake. Kiongozi anayekuwa mfano wa nidhamu, uwajibikaji na uadilifu huwa na ushawishi mkubwa kwa wengine.

Kwa kifupi, jiulize: ungependa kufuata kiongozi wa aina gani? Kisha jitahidi kuwa mtu huyo. Kwa ujumla, kuwa kiongozi si suala la cheo au mamlaka, bali ni uwezo wa kuathiri watu kwa njia chanya. Mtu yeyote anaweza kujifunza uongozi kwa kukuza tabia kama uwajibikaji, uaminifu na uwezo wa kufanya kazi na watu wengine.

Katika dunia ya leo inayohitaji ushirikiano na ubunifu, jamii inahitaji viongozi zaidi wanaojengwa juu ya maadili, si mamlaka pekee. Habari njema ni kwamba uongozi ni stadi inayoweza kujifunzwa—na safari yake huanza pale mtu anapoamua kubadilisha tabia zake na kuwahudumia wengine kwa dhati.